GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **255** R/Awwal-R/Akhir **1447** AH Septemba– **2025** Ikha **1404** HS BEI TSH 800/=

HATIMA YA WAPINZANI WA SEYYIDNA AHMAD AS

(SH. MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII NA ABDULLAH ATHAM) KUSHINDWA KWA MAADUI

Na: ***Na Hassan Sango na Alhaj Mahmood Hamsin Mubiru.***

Muhubiri wa Islam Ahmadiyya asiyechoka na wakati wote amebeba uso wa tabasamu. Mwenye mahaba ya kusoma na kujiendeleza. Muadilifu katika uwanja wa siasa unaoitwa mchafu nae akautakasa mchezo huo. Kazi ya Jamaat kwake ndiyo ikawa furaha. Ukhalifa ndio kiini cha Islam. Sifa zote hizi ukizichanganya ndipo unapopata picha ya ndugu yetu aliyezaliwa mwaka 1950 na kututoka siku ya Eid-Ul-Adh'a tarehe 07/06/2025 Moshi Mohammed Mlekeakule wa Nguruka Kigoma. Sisi ni Wa Allah na Kwake Tutarejea.

Mambo yote unayoyafanya hapa duniani, yanapotea mithili ya moshi isipokuwa unayoyafanya kwa dhati ili kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Bila shaka ni wachache sana kama wapo watakaomkumbuka Bw. Moshi Mohammed Mlekeakule, kuwa alikuwa mjenzi mzuri wa nyumba na fundi seremala lakini hakuna atakayesahau hata kwa sekunde moja mapenzi yake ya kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) kwa watu wote. Wakati wote alikumbuka wajibu aliopewa kila Ahmadiyya na Khalifatul Masihi -II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) aliyesema; "Kila Ahmadiyya ni Mhubiri na Balozi wa Ahmadiyya".

Moshi Mohammed alikuwa na mtizamo uliozama kuhusu mahubiri. Hii ni kazi takatifu walioifanya Manabii na hakuna kazi inayoweza kuwa bora kuliko hii. Hata hivyo kazi hii ina sehemu yake ya pili. Ina uchungu na inahitaji uvumilivu ambao umejengeka kwenye imani iliyo imara. Si rahisi hata kidogo kufanya kazi hii bila kuwa na msaada wa Allah. Siku zote kabla ya Kwenda kwenye mahubiri alikuwa na desturi ya kufanya maombi ili Allah Amsaidie. Binadamu tulivyo dhaifu tunaweza kufanya nini bila ya msaada wa Allah. Ni silaha ambayo imetumika sana na Wanajamaat ambao wameacha jina katika uwanja wa mahubiri. Walielewa udhaifu wao na hivyo kumuomba Allah Awaimarishe katika kutimiza maangamizi, na maangamizi ya namna hii yanapatikana kwa kuwa adui wa wajumbe wa Mwenyezi Mungu. Watungaji wa uongo juu ya Allah, kwa muujibu wa kurani, hawawezi kufaulu, vile vile wale

UK. 05

Ilikua siku ya Jumamosi muda wa Adhuhuri siku ya Iddul Adhha nikiwa katika kufanya mahubiri ya kugawa vipeperushi nasikia simu inaita napokea nasikia sauti ya mtu analia na kusema innaillahi wainnaillah rajiun, Ilikua sauti ya Mwalimu wa Mkoa wa Kigoma akisema kuwa Mzee Moshi Muhammad amefariki mchana huu akiwa Hospitali ya Nguruka hivi Nijiandaa Kwenda.

Pamoja na kusikia huzuni Sana sikuacha kugawa vipeperushi kule eneo la Gongo lamboto Dar esalaam, Kwani Mzee Moshi alipenda Mara kadhaa kunielezea maneno ya Maulana Sheikh Muhammad Munawwar aliyepata kuwa Amir na Mbashir mkuu wa Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya Tanzania aliyethamini sana kazi za Jamaat alisema kuwa akifa baada ya kuzikwa kwake

MOSHI MUHAMMAD MLEKYAKULE MSIMBE AMEAGA DUNIA

kama kuna uwezekano kazi za Jumuiya Ahmadiyya ziendelee bila kusimama muda mrefu kwa sababu ya msiba.

Mzee Moshi Mohammad alizaliwa Nguruka eneo la Izimbwa mwaka 1950 ambalo lipo Ng'ambo ya ziwa Sagara na hatimaye walihamia Mambwe upande wa pili wa ziwa hilo na kisha kuhamia Itebula ambako ni karibu sana na Nguruka mjini .

Safari yake ya kujiunga na Jamaat Ahmadiyya ilianzia Itebula mwaka 1968 ndugu mmoja aitwaye Matata Kipeta aliyetembelea kijijini akitokea Wilaya ya Mpanda alipo muhubiria na kufanikiwa kujiunga na Jamaat Ahmadiyya, Wakati huo Mzee Moshi alikua Kijana wa takriban miaka 18 tu.

Baada ya kujiunga na Jumuiya tukufu ya Masihi aliye ahidiwa

UK. 07

KWA MOLA AMEREJEA

Muhubiri wa Islam Ahmadiyya asiyechoka na wakati wote amebeba uso wa tabasamu. Mwenye mahaba ya kusoma na kujiendeleza. Muadilifu katika uwanja wa siasa unaoitwa mchafu nae akautakasa mchezo huo. Kazi ya Jamaat kwake ndiyo ikawa furaha. Ukhalifa ndio kiini cha Islam. Sifa zote hizi ukizichanganya ndipo unapopata picha ya ndugu yetu aliyezaliwa mwaka 1950 na kututoka siku ya Eid-Ul-Adh'a tarehe 07/06/2025 Moshi Mohammed Mlekeakule wa Nguruka Kigoma. Sisi ni Wa Allah na Kwake Tutarejea.


Mambo yote unayoyafanya hapa duniani, yanapotea mithili ya moshi isipokuwa unayoyafanya kwa dhati ili kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Bila shaka ni wachache sana kama wapo watakaomkumbuka Bw. Moshi Mohammed Mlekeakule, kuwa alikuwa mjenzi mzuri wa nyumba na fundi seremala lakini hakuna atakayesahau hata kwa sekunde moja mapenzi yake ya kufikisha ujumbe wajibu huo wa lazima. Kuna mitihani mingi katika mahubiri na historia ya Ahmadiyya inao Ushahidi. Sheikh Saleh Mbaruku Kapilima huko Njinjo zilifanyika harakati za kuondoa uhai wake. Mwalimu Matimbwa aliwekwa kwenye gunia na kutupwa kutoka juu ya

UK. 03

TABASAMU LA KWELI LA DR. HAMIDU S. JAKA SAHIB

Na. Alhaj Mahmood Hamsin Mubiru

Tabasamu linalotoka kwenye sakafu ya moyo na kuganda kwenye uso, Rais wa Madaktari Waahmadiyya Tanzania, mahaba ya dhati kwa Jumuiyya, kuwaenzi na kuwaheshimu wazazi, kuwatumikia wote akiongozwa na falsa 'Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote'. Ukichanganya sifa zote hizi ambazo



UK. 09

MAJIBU KWA MASALAFI

UK. 04

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MUUJIZA

Yapo mambo hata bila kufikiri sana, hautakuwa na neno la kusema isipokuwa neno 'muujiza'. Tafadhali chukua fikra zako hadi iliyokuwa ikiitwa 'Hijaz'. Kwa jicho la akili yatazame majabali ya kutisha, ardhi isiyokuwa na mti, mchanga mtupu, na mji maarufu ukiwa Maka. Huu ni mji ambao ustaarabu haujawahi kubisha hodi. Ni ushirikina mwanzo mwisho. Wanaojua kusoma na kuandika unaweza kuwahesabu kwenye kiganja za mkono. Shughuli ya watu hao ni kamari, ufuska, pombe, dhuluma, uonevu, n.k hilo ndilo shuka lililofunika ambako kuna nyumba ya kwanza ya Allah kwa ajili ya ibada.


Tuma tena akili zako, na kutana na bwana ambae katika giza hilo ni mtu ambae kwa macho yetu sisi hajui kusoma wala kuandika. Lakini anaheshimika kwa huruma na ukweli wake. Kwa tabia hiyo anapewa lakabu ya Al-Amini. Na hata anapowakusanya jamaa zake kueaeleza ujumbe alio nao; "Je nikiwaambia nyuma ya mlima huu kuna jeshi kubwa linakuja kuwashambulia, mtaniamini?" wote kwa sauti moja wanaitikia 'Swadakta'. Lakini tazama la kushangaza, anaposimama na kuwaambia kuwa; "Nimepokea ujumbe kutoka kwa Allah kwamba Allah ni Mmoja ni Yeye pekee ndiye Anayestahili kuabudiwa". Hapo wanakuja juu kama moto wa kifuu.

Maneno ya Allah yanazidi kuteremka kwa takribani miaka 23. Huyu asiyejua kusoma na kuandika anayakumbuka maneno yote hayo na anawaeleza kuwa uzima na maendeleo vyote vimo katika maneno hayo.

Yeye anaelekeza mpangilio mzima wa Qur'an Tukufu, watalaam wa baadae wanashangaa kuhusu mpangilio huu. Kuna mtiririko wa ajabu usio na dosari. Maneno hayo aliyoteremshiwa yanapewa ahadi, ahadi ambayo haijawahi kupewa kitabu chochote kingine, ahadi ya ulinzi; "Sisi ndio tulioteremsha na Sisi ndio tutakaolinda". Na miaka zaidi ya 1400 watalaam na watafiti wanakuna vichwa na hatimae wanakubali hakuna kilichopungua au kutoweka katika Qur'an Tukufu. La kushangaza zaidi, waandishi wa vitabu vingine wanakiri udhaifu wao mwanzoni tu mwa vitabu vyao, Qur'an Tukufu mwanzoni inatangaza kuwa Aliyeiteremsha ni Anayejua sana na hakuna shaka yoyote katika kitabu hicho. Mabadiliko yote yanayotokea duniani hayajawahi na hayatawahi Kwenda kinyume na Qur'an Tukufu. Sababu ni kwamba Aliyeumba Dunia na kanuni zake ndiye huyo huyo Aliyeteremsha Qur'an Tukufu.

La kushangaza zaidi ni kwamba kuna watu katika kila pembe ya Dunia ambao wanatembea na Qur'an Tukufu nzima vifuani mwao. Ushabiki weka kando, nipe Habari ya kitabu chochote cha kidini ambacho kimehifadhiwa na waumini wa kitabu hicho. Qur'an Tukufu inapendwa na sehemu za kitabu hicho zinasomwa mara tano kila siku bila kusahau wale wanaoamka usiku kusali Tahajjud.


Kama umekuja duniani, na Allah Akakujaalia akili na macho na hukuweza kugundua muujiza huu wa Qur'an Tukufu basi ujihesabu u miongoni mwa wenye hasara. Ila Habari njema ni kwamba usikate tamaa. Fursa bado ipo ya kuona muujiza huu wa Qur'an Tukufu. Aliyeuweka bayana muujiza huu ni Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as], mpokee ili uweze kupokea muujiza huu wa Qur'an Tukufu.



QUR'AN TUKUFU

وَقَضٰى رَبُّكَ اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّآ اِيَّاهُ
وَبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا ؕ اِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ
الْكِبَرَ اَحَدُهُمَآ اَوْ كِلٰهُمَا فَلَا تَقُلْ
لَّهُمَآ اُفٍّ وَّلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَّهُمَا
قَوْلًا كَرِيْمًا ۝

24. Na Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu ye yote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi; kama mmoja wao akifikia uzee ukiwa naye, au wote wawili, basi usiwaambie hata aakh wala usiwakemee, na useme nao kwa msemo wa heshima.



NUKUU YA HADITHI

Kutoka kwa Abu Hurairah, kutoka kwa Mtume[saw] alisema: "amedhalilika, tena amedhalilika, tena amedhalilika!" Akaulizwa: "Nani huyo, ee Mjumbe wa Allaah?" Akasema: "Yule ambaye amewakuta wazazi wake wawili wanazeeka, mmoja wao au wote wawili, naye asiingie Peponi."



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Yeyote yule asiyewaheshimu wazazi wake na asiyewatii katika mambo yanayojulikana vizuri ambayo hayako kinyume na Quran, na asiyejali kuwahudumia, hayuko miongoni mwa jumuiya yangu." ***(Kashti e Nuh', Ruhani Khazain, Vol. 19, ukurasa wa 19)***

Kuwahudumia wazazi ni tendo zito sana. Imeteremshwa katika Hadith Tukufu kwamba watu hao ni wenye bahati mbaya sana: mmoja ni yule aliyepata Ramadhani na Ramadhani ikapita lakini dhambi zake hazikusamehewa, na wa pili ni yule aliyewakuta wazazi wake na wazazi wake wakaaga dunia lakini dhambi zake hazikusamehewa. Mtoto anapokuwa chini ya kivuli cha wazazi wake, huzuni na masikitiko yake yote hubebwa na wazazi. Mtu anapojishughulisha mwenyewe na mambo ya kidunia, ndipo anatambua thamani ya wazazi. Mwenyezi Mungu amewaweka mama na baba mbele katika Quran Tukufu kwa sababu mama huvumilia maumivu makali kwa ajili ya mtoto. Huu ni upendo wa asili, ambao hakuna upendo mwingine unaoweza kushindana nao. Mwenyezi Mungu ameashiria hili katika Quran Tukufu, akisema, 'Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na wema na kuwapa jamaa' (Surah An-Nahl 91:16)." (Malfoozat, Juzuu ya 7, ukurasa wa 375, iliyochapishwa 1934)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Aziz Ahmad Ng'amilo
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

KWA MOLA AMEREJEA

Kutoka uk. 01

nyumba. Rufiji walinyang'anywa wake. Mzee Ndendekele, Kibindu, Mlandula, Namwete, Mahadhi Mwinshaweji, Adili Damani, Iddi Ramadhani, Rashidi Msabaha, Bakari Rashidi Kazema, Sheikh Kaluta Amri Abedi, Mtamila, Mbiyana, Mbambwa, Jimpota, hawakuwa tayari kunyamazishwa. Licha ya hila na vitimbwi vingi. Moshi Mohammed Mlekeakule aliwasha moto Nguruka na vitongoji vyake. Kazi hiyo aliifanya peke yake. Masheikh walikasirika kwa kazi aliyokuwa anafanya na malalamiko hayo waliyapeleka polisi. Moshi Mohammed aliitwa na wale Masheikh wakatishia kuwa usipoacha mahubiri hayo kitakachokupata ndugu zako wasilalamike. Kwani hiyo ni kaburure -ugonjwa wa kujitakia. Acha kabisa! Walitishia, au utakufa. Moshi Mohammed kwa ushujaa alisema; "Uzima huu hamkunipa nyinyi, na nyinyi hamuwezi kuondoa uzima huu, nitaondoka Atakapopenda Yeye". Moshi aliondoka na huko nyumbani alifanya maombi mfululizo. Alimuomba Allah Ayarefushe maisha yake ili Masheikh hao wa vilemba wasiweze kuranda kwa kumkebehi. Na kweli maombi yalikubaliwa na Masheikh wale wote wakapukutika na kumuacha Moshi Mohammed Mlekeakule akidunda. Hadi alipofariki miaka mingi baada ya tishio lao.

Wakati yupo Dar es salaam na wakati huo Amir na Mbashiri Mkuu alikuwa Maulana Sheikh Jamil Rahman Rafique, Moshi Mohammed hakukosa asilani Msikitini hususani siku ya Jumapili. Hizo zilikuwa enzi njema za kubeba vikapu na kueneza mafundisho sahibi ya Islam. Harakati hizo ziliendeshwa na Sheikh Jamil Rahman Rafique sahib aliyeonesha mapenzi makubwa katika kazi hii ya mahubiri. Siku hiyo ya Jumapili tulimkuta tayari yuko ofisini na kuongoza maombi kabla ya kuondoka. Hakuishia hapo alitusindikiza hadi kwenye lango kuu na tuliporudi alitupokea kwa shangwe na maji baridi. Harakati zote hizo zilimpa fursa Moshi Mohammed kujifunza. Baadhi ya wasomi wazuri Dr. Iddi Ibrahim Mwanga sahib, Alli Saidi Mosse sahib, Mohammed Saidi Kibindu sahib, Abdulrahman Mikila sahib, Ramadhani Abdallah Marunda sahib hawa wote hawakukosa kwenye Tabligh. Imani yake bw. Moshi Mohammed juu ya Ahmadiyya imeongezeka. Huwezi kubeba kikapu chenye vitabu ukipita huku unazomewa na watu kama huna Imani thabiti. Huu ndio umekuwa mwenendo wa wasomi wengi wa Jumuiyya kutanguliza dini mbele ya kila kitu. Alikuja kujifunza baadae kuwa wasomi wakubwa ndio walikuwa wanashughulika katika kuwahudumia watu, kuosha vyombo, n.k katika Jalsa Salana ya huko Rabwah na London.

Kuna tukio alilolisikia ambalo halikutoka kichwani mwake daima. Mwaka 1941 Hadhrat Chaudhry Muhammad Zafrullah Khan (ra) aliteuliwa kuwa Jaji katika Mahakama Kuu ya India. Wakati huo Khalifatul Masih-II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) alianzisha mpango wa kuwaita Wanajamaat wajitolee na Kwenda kuhubiri vijiji Jirani na Qadian. Akiongozana na Wabashiri wa Jamaat mwaka 1941-1942 alizunguka katika vijiji hivyo akihubiri na hata dakika moja haikumjia ya kwamba yeye ana cheo kikubwa. Mtu wa kawaida angejiuliza, watu wasikiaje kwamba nilienda kuhubiri katika vijiji maskini kama vile Depai, Bheen na Athwaal na huko kote alipita akiwa mtumishi mnyenyekevu wa Ahmadiyya. Ikumbukwe Allah Alimruzuku sana Hadhrat Chaudhry Muhammad Zafrullah Khan (ra) katika maisha hayahaya ya dunia yanayotafutwa na wengi. Alikuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa kwanza wa Jamhuri ya Kiislam ya Pakistan iliyoanzishwa mwaka 1947. Alikuwa Balozi wa kudumu wa Pakistan katika Umoja wa Mataifa na huko akawa binadamu wa kwanza kusoma Suratul Fatiha katika Baraza la Umoja wa Mataifa bingwa wa kutetea haki za Wapalestina. Alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Dunia huko 'The Hague'. Ameandika vitabu vingi kuhusu Islam. Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) Pamoja na Sir Hadhrat Chaudhry Muhammad Zafrullah Khan (ra) ndio wametumia kalamu zao katika kuhifadhi historia iliyotukuka ya Ahmadiyya. Ilikuwa ni matukio hayo na historia ya Sir Hadhrat Chaudhry Muhammad Zafrullah Khan (ra) vilivyootesha mbegu katika ardhi yenye rutuba ya Moshi Mohammed, kwa kuzingatia mifano hiyo kila aliposafiri Kwenda mahala popote hakusahau kubeba Mapenzi ya Mungu na vipeperushi vya Jamaat huko alivigawa na kuuza gazeti la Mapenzi ya Mungu. Kiwanda chake cha Useremala kiligeuka uwanja wa mahubiri. Ni bidii hizi zilizomfanya mkoa wake uwe mara kwa mara ukiongoza na kujinyakulia Zawadi za mahubiri. Kilele cha mafanikio yake katika mahubiri ni muhadhara wa Nguruka ambao kwa ujumla wake mipango yote alianzisha, kuiratibu na kuikamilisha. Barua, mipango, hivyo vyote alivibeba na hatimae mjadala ukafanyika ambao umeacha athari kubwa katika uwanja wa mahubiri. Masheikh wa Nguruka na wengine kutoka Kigoma Ujiji walikusanyika na jeshi la Waahmadiyya liliongozwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durani sahib aliyekuwa Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania akiwa Pamoja na Sheikh Bakri Kaluta sahib na Sheikh Daud Ahmad Mmoto sahib. Wanajamaat Waahmadiyya wa Dar es

salaam walishiriki katika mhadhara huo. Maisha yote ya Moshi Mohammed yanatukumbusha ukweli ya kwamba Ahmadiyya mzuri ni yule anayetoa kipaumbele kwa mahubiri na kuwa Balozi mzuri wa Ahmadiyya kwa maneno na vitendo.

Toka Msikiti Masjid Salaam ufunguliwe mwaka 1957 kimekuwa ni kituo cha kutoa elimu. Upo wakati watu walikuwa wanakuja kujifunza Kiarabu, Kiingereza na Mashairi. Sheikh Muhammad Munawwar sahib na Sheikh Jamil Rahman Rafique sahib waliendesha masomo ya lugha ya Kiarabu. Sheikh Jamil alituhimiza kuwa kila anayejua amfundishe mwingine. Masomo ya lugha ya Kiingereza yakaanza na yalikuwa chini ya Mwalimu B.K. Kheri sahib. Darasa hilo liliendelea ingawaje si kwa nguvu sana. Na hapo ndipo zilipoonekana juhudi za Moshi Mohammed za kutaka kuongeza elimu yake. Alikuwa na hamu kubwa ya kujifunza lugha ya Kiingereza akiwa na shabaha ya kusoma vitabu vya Jumuiyya ambavyo vimeandikwa katika lugha ya Kiingereza. Nakumbuka hakukosa katika somo hilo la Kiingereza. Kwa ujumla kusoma kulikuwa ndicho kikombe chake cha kahawa. Alipenda sana kusoma vitabu vya Jamaat na vile vya nje ya Jamaat. Hakukosa hata kidogo gazeti la Mapenzi ya Mungu kwa kulisoma na kulieneza. Ameandika Makala nyingi katika gazeti hilo na kuchangia katika bustani ya Washairi. Ni kutokana na bidii ndipo alipoanza kujifunza utungaji wa mashairi. Alipenda sana kutembea na kitabu cha 'Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri'. Shairi alilolipenda sana ni lile la 'Wamchao Rahmaan ndio wenye mwisho mwema' la sheikh Amri. Bidii ya kutaka kujifunza na usomaji wa vitabu ni mambo mawili ambayo tunayahitaji sana kwa hivi sasa. Utamaduni wa kujisomea umepungua sana licha ya ukweli ya kwamba tunavyo vitabu vingi vya Masihi Aliyeahidiwa (as) na Jumuiyya kwa ujumla katika lugha ya Kiswahili. Tunalo deni kubwa la shukrani kwa Sheikh Mubaraka Ahmad sahib, Sheikh Muhamamd Munawwar sahib, Sheikh Jamil Rahmaani Rafique, Sheikh Muzaffar Ahmad Durani sahib, Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya sahib, Sheikh Bakri Kaluta sahib, Mwalimu Hemedi Feruzi Mahmudu Mbiyana sahib, Mwalimu Bakari Rashidi Kazema sahib na Muhammad Saidi Kibindu sahib. Wanazuoni wetu hawa daima aliwashukuru na kuwaombea kwa kazi nzuri ya kuweka maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) na Wanazuoni wengine katika Kiswahili.

Tunaweza kuwashukuru Wanazuoni wetu hao kwa kusoma vitabu hivyo na kuzingatia yaliyomo.

Katika ulimwengu ambao hauna hofu na Allah, zifuatazo ni sifa ambazo unatakiwa kuwa nazo katika uwanja wa siasa. Unafiki uliopitiliza, kusema jambo moja jukwaani na Kutenda jingine unaposhuka jukwaani, kila siku kupiga kelele kuwa upamoja na wanyonge na ni mtetezi wao kumbe unatetea tumbo lako, kila anayesimama mbele yako akiwa ni kikwazo unamuondoa njiani kwa njia yoyote ile, ubingwa wa kueleza kuwa umefanya kadhaa wa kadhaa wakati shughuli zinatokana na jasho lao kwani wanalipa kodi, kuwa na mahaba makubwa ya kukusanya mali, rushwa ya kila aina ndio mwenendo wako, kujipendekeza ufikie malengo yako, ni vigumu katika ulimwengu wa hivi leo kuingiza taqwa katika siasa kama ilivyo vigumu kwa tembo kupita katika tundu la sindano. Siasa ni mchezo wa wale ambao ni mabingwa wa kutumia silaha ya ulimi na ukosefu mkubwa wa vitendo. Moshi Mohammed alikuwa ni mwanasiasa aliyejitahidi Kutenda haki na kuwa muadilifu. Alitambua kuwa kwa kila tendo lake, kesho itambidi atoe maelezo. Yeye alijihesabu ni mtumishi na mtumishi hawezi kuwa bora kuliko aliyemuajiri. Uwezo wake wa kujichanganya na watu kulimfanya apendwe sana na akaheshimiwa. Hata katika chama chochote alichoingia hakufuata mkumbo, yeye alichotaka ni hoja zinazotolewa. Moshi Mohammed alisema kwamba inawezekana kabisa siasa kuwa mchezo safi ikiwa kuna hofu ya Mwenyezi Mungu. Ni ajabu ya kwamba katika siasa ya vyama vingi pale Nguruka aliheshimika kwa viongozi wa vyama vyote na walimkimbilia kila walipohitaji ushauri. Alikuwa mbali na majivuno na nyumba yake ilikuwa wazi wakati wote. Wanasiasa wanachojali ni maslahi sio usafi wa moyo. Ukiona umekuwa kiongozi mahala Fulani na unafahamika kuwa ni Ahmadiyya ukapendwa na kuheshimiwa na wengi basi tambua umekwenda maili moja zaidi katika wema. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Moshi Mohammed na Ushahidi ni umati wa watu waliomiminika katika mazishi yake.

Moshi Mohammed maisha yake yote alikuwa ni mjenzi wa nyumba na fundi seremala. Na mara kwa mara alipata fursa ya Kwenda kufanya kazi mahali pengine. Hapo ndipo Imani yake iliweza kujidhihirisha kwa uwazi zaidi. Hata kama anapata pesa kiasi gani alipoitwa na Jamaat aliacha kazi hiyo na

kwanza afanye kazi ya Jamaat. Wakati akifanya kazi ya Jamaat alipendelea kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Kutumikia Jamaat kwa bidii na maarifa na kuchukua pesa kidogo kama posho yake. Jumuiyya ilimuamini sana na ndiye aliyepewa kazi ya kuweka vigae katika Msikiti wa Tabora -Alfazal ambao ni Msikiti wa kwanza wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Tanganyika uliofunguliwa na Sheikh Mubarak Ahmad mwaka 1944. Kazi hii aliifanya vizuri. Alitumikia Jumuiyya katika sehemu zifuatazo; Dar es salaam, Morogoro na Dodoma. Katika maisha yake hayo ya ujenzi na useremala aliwafundisha baadhi ya Wanajamaat na kuwapata fani zake hizo na hivi leo Wanajamaat hao wanaendesha maisha yao kupitia fani hizo. Umekuwepo utamaduni wa Wanajamaat kusaidiana katika suala zima la kupata riziki. Wanajamaat wanasaidia Wanajamaat wenzao. Mapenzi ya aina hii ni muhimu katika maendeleo ya Jamaat kwani ni muhimu kukumbuka anavyosema Allah katika Qur'an Tukufu, kuwa 'Waaminio ni wenye kuhurumiana wao kwa wao'.

Moshi Mohammed alikuwa na mfungamano na Ukhalifa. Ukifika wakati wa kusikiliza hotuba ya Ijumaa ya Khalifa Mtukufu yeye anakuwa mtu wa kwanza kufika ilipo runinga. Kwa hakika kuna waraka umetoka unaowataka wote walio katika mazingira ya Msikiti kutojishughulisha na shughuli zozote zile isipokuwa hotuba ya Huzur Anwar[atba] pindi akiwa anahutubia. Moshi Mohammed aliamini kuwa hakuna njia rahisi ya kupata elimu ya kimbingu kwa hivi sasa isipokuwa kumsikiliza Khalifa wa Mwenyezi Mungu. Mafanikio yote yanayoonekana na kufanywa na Jumuiyya, uchapishaji wa vitabu, usambazaji wa Wabashiri sehemu nyingi za dunia, ujenzi wa Misikiti, kusaidia binadamu kupitia Humanity Firsty, mashule, hospitali, magazeti, MTA, muujiza huu mkubwa wa kutumikia Islam kwa kiwango hicho siri yake ni Ukhalifa. Wale wanaoshikamana na Ukhalifa ndio wanaopewa msaada wa kumtumikia Allah. Moshi Mohammed alikuwa na mapenzi makubwa na Ukhalifa. Nchi yetu ilipopata baraka za kutembelewa na Khalifa wa Allah kwa mara ya kwanza, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad[rh] mwaka 1988 Moshi Mohammed alifika jijini Dar es salaam kutoka Nguruka wiki mbili kabla ya na hivyo kushiriki kwenye matayarisho ya kumpokea Khalifa Mtukufu. Khalifa wa tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] alipotembelea Tanzania Bw. Moshi Mohammed alishiriki katika mapokezi ya kumpokea Khalifa Mtukufu. Maisha ya Moshi Mohammed yalitawaliwa na kutimiza haki za Allah na viumbe wake. Ni shabaha inayofanya maisha yake yawe na maana. Hakuna ufaulu mkubwa kuliko huo. Allah Utujaalie nasi kuipata shabaha hiyo.

… Mwisho …

MAJIBU KWA MASALAFI

Kutoka Uk wa 1..

Kwenye kijarida chake ameandika "Mirza Ghulam Ahmad anamaradhi mengi, mpungufu wa akili na anatumia madawa ya kulevya (cocaine)" uk 1.

Nikijibu shutuma hizi tatu :
i)Ana maradhi mengi
ii) Mpungufu wa akili
iii) Anatumia madawa ya kulevya

Nianze na "ana maradhi mengi. "Maradhi kwa mwanadamu ni jambo la kawaida , lakini hebu msome huyu mwenye maradhi mengi alivyofanikiwa katika Nyanja zote . Ameishi maisha safi na ameutetea Uislamu maisha yake yote .
Ameweka misingi madhubuti ya Jumuiya ya Ahmadiyya ambayo imeshaenea duniani kote kwa msaada wa Allah (sw) . Yeye Abu Halima ni shahidi juu ya hili , amekiri kwenye kijarida chake kama alivyo andika :

"Makadiani wengi kwa sasa wanapatikana nchini India na Pakisatani , na wachache kati yao hupatikana Israel na nchi za Kiarabu "(uk 4)
Kwa taarifa ya wasomaji wetu, mpaka naadika makala hii, Ahmadiyya ina vituo katika tkribani mataifa 240 duniani kote ikiwemo Tanzania.
Akishuhudia maendeleo haya Abu Halima ameandika:
"Vituo vyao vipo sehemu nyingi ikiwemo Amerika, Ulaya na Afrika na pia wana vituo katika nchi za Kiarabu kama vile Kuwait, Bahrain, Muscat, Misri, Dubai, Sharja, Jordan na Syria "(uk 4)
Hiyo ndio kazi ya Yule anayemsema Abu Halima kwamba "Ana maradhi mengi"
Hebu twambie ewe Abuu Halima mwenye afya tele unafanya kazi gani inayosaidia Uislamu?
Na sasa niingie kwenye nukta ya "mpungufu wa akili" Katika lugha ya Kiarabu, mtu wa aina hii huitwa "***Majnuun***" .Basi ujue ewe msomaji mpendwa kwamba, hiyo ndiyo SUNNA ya Manabii wote. Watu wa Nuhu[as] walisema
"HUYU SIYE ILA NI MTU MWENYE WAZIMU"
(Sura Almuuminuun 23 : 26)
Firauni naye alisema kuwa Nabii Musa ni mpungufu wa akili (Majnuun)
(Firauni) akasema:-
"BILA SHAKA MTUME WENU ALIYETUMWA KWENU NI MWEHU"
(Sura Ash – shua'raa, 26 : 28)
Mtume Muhammad (saw)na yeye aliambiwa hayo hayo
"EWE ULIYETEREMSHIWA MAWAIDHA HAKIKA WEWE NI MWEHU"
(Sura Al – Hijri 15 : 7)
Lakini Allah[saw] Anasema:
"NDIVYO HIVYO HAKUNA MTUME YOYOTE ALIYEWAFIKIA WALE WA KABLA YAO ILA WALISEMA HUYU NI MCHAWI AU MWEHU"
(Adhariyat 51 : 53)
Kwa hivyo hatumshangai Abu Halima kumwita Sayidna Ahamad mpungufu wa akili, hiyo ndiyo kawaida ya watu hao ambao Allah[saw] amewaita" WATU WAHALIFU"
(Surat Adharyat 51 : 54)
Na sasa niingie kwenye nukta ya tatu" Anatumia madawa ya kulevya" (uk 1)
Tunamuuliza Abu Halima pamoja na Mashekhe aliorejea kwao, je wanao ushahidi juu ya jambo hili? au ni inadi tu iliyomo mioyoni mwao? Basi jibu ni lile lile ambalo nimeliandika kwenye sura ya pili kwamba kilicho haramishwa kwenye Kur-an tukufu hatuwezi kukihalalisha, na wala kilicho halalishwa humo hatuwezi kukiharamisha . Hatuna ujasiri huo. Pengine Mawahaby/Masalafi wanao ujasiri huo au zaidi ya huo, maana wamehalalisha damu za Waislamu:-
"Imefika pahala wakikamia kuwauwa Waislamu wenzao wasiamini katika madhehebi yao. Na hilo si ajabu maana ndivyo alivyofanya Muhammad Abdul-Wahab, kuuwa Waislamu waliompinga."
(Upotovu wa Uwahaby uk. 20)

SURA YA NNE
CHEO CHA MIRZA GHULAM AHMAD[AS]
Katika kijarida chake Abu Halima ameandika:
"Kisha akazidisha katika upotevu wake huo mpaka akafikia kudai kuwa yeye ni MAHDI ambaye shia ithnashiria wanamngojea." (ukurasa wa 2)
Naam na hicho ndio hasa cheo chake Mirza Ghulam Ahmad[as].
Yeye ndiye Masihi aliyeahidiwa kwa jina Issa bin Maryam, maana vyeo hivyo viwili ni vya mtu mmoja kwa kauli ya mtukufu Mtume[saw]
"LAA MAHDI ILLAA ISSA"
Rejea (Ibnu Majah , Baab shiddatu zaman uk. 257 na Kanzul ummal j.7 uk 186)
Tafsiri ya hadithi hiyo ni kwamba "Hakuna Mahdi isipokuwa Issa" msimuliaji wa hadithi hii ni Muhammad bin Khalid Al-Jundiyy. Imam Shafi[Rha] ameipokea kutoka kwake Al- Jundiyy[Rh a]
Na Yhaya bin Muiin amesema kwamba Muhammad bin Khalid Al – Jundiyy ni msimulizi mwenye kutegemewa. (Rejea Tah'dhib Tah'dhib uk 144).
Na Mtume[saw] alishasema zamani kwamba Imam Mahdi atatokea katika kijiji cha Qadiyan soma hadihti hii.
"Mahdi atatokea katika kijiji kiitwacho Qad'a na Allah atamsadikisha kwa ishara, na atawakusanya maswahaba wake sawa na idadi ya walioshiriki vita vya Badri. Watu mia tatu na kumi na tatu. Na atakuwa na sahifa iliyopigwa muhuri ambamo mtakuwa na majina yao pamoja na miji yao"
(Rejea: Irshadat Farid, J 3 uk 70)
Kuhusu muda wa kudhihiri imamu Mahdi, Mtume[saw] amesema
"Itakapopita mika elfu moja mia mbili na arubaini (1240)Allah atamtuma Mahdi"
(Annajmu Thaaqib, j 2 uk 209)
Kumbuka ndugu msomaji wa makala hii, huko nyuma nimeshaandika kwamba Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] amezaliwa tarehe 14 shawal 1250 Hijria mpaka muda naandika makala hii huu nimwaka wa 1446 Hijria. Maana yake ni kwamba muda alioutaja Mtume[saw] wa kudhihiri imamu Mahdi umeshapita na aliyejitangaza kwamba yeye ndiye imamu Mahdi ni Mirza Ghulam Ahmad[as] pekee. Hivyo unalazimika kumuamini au vinginevyo uamini kwamba Mtume amesema uongo (Mungu apishe mbali)
Kuhusu cheo cha Imam Mahdi na Isa bin Maryam ,amekitaja Mtume[saw] kwa kusema.
"Na Nabii wa Allah Isa pamoja na masahaba zake watazungukwa na maadui, kisha Nabii wa Allah Isa na masahaba wake watamuelekea Allah.
Kisha Nabii wa Allah na maswahaba zake watashukia mahali Fulani.
Kisha Nabii wa Allah na maswahaba zake watamuekea Allah"
Rejea katika Muslim, bab dhikru Dajjal)
Yeye ni Mtume (Rasuul) ambaye hana sheria . Anaisimamia sheria iliyopo kwa vile yeye ni khalifa wa Mtume[saw].
Amesema Mtume[saw] "Sikilizeni, hakika hamna Nabii baina yangu mimi na yeye Isa bin Maryam. Sikilizeni, huyo ndiye KHALIFA wangu katika umati wangu. Sikilizeni huyo ataua Dajjali na kuvunja msalaba na kuondoa Jizya. Vitakwisha vita (vya dini) Sikilizeni, yeyote apatae kuonana naye amtolee salamu"
Rejea katika Twabaraniil – Ausat wasswaghir)
Hadithi hiyo hapo juu inajibu pia hoja ya Abu Halima juu ya jihadi
Ameandika
"Wanatoa wito wa kutokomeza itikadi ya waislamu kuamini JIHADI" (Ukurasa wa 11)
Kwa hakika katika jihadi hii anayoitaka Abu Halima haina nafasi katika wakati huu wa Masihi aliyeahidiwa.
Hdithi yahapo juu ni moja wapo ya hadithi zenye ushahidi wa jambo hili lakini bado zipo JIHADI mbili:
JIHADI KUBWA - Kufikisha ujumbe (Tabligh)
JIHADI KUU - Kila mtu kupigana na nafsi yake .Hivyo ndivyo Mtume[saw] alivyoelekeza.

SURA YA TANO
MTETEZI WA UISLAMU
Abu Halima tangu ukurasa wa kwanza wa kijarida chake ameanza kunungunika kwamba Utume wa Sayidna Ahmad[as] ni ajira kutoka kwa Waingereza, ameandika
"*Akachaguliwa na kupewa jukumu la kudai Utume*" (uk 1)
Maneno yanayofana na haya , aliambiwa Mtume Muhammad[saw].
Soma aya hii:
"NA WAKASEMA WALE WALIOKUFURU SIO HUU ILA NI UZUSHI ALIUZUSHA NA WANAMSAIDIA JUU YAKE WATU WENGINE ....."

(sura Al-Furqaan, 25 : 5)
Basi na Abu Halima naye amenaswa na aya hiyo bila kujua. Hakika yenyewe ni kwamba, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[saw] alisema kwamba, si haki kupigana na serikali ambayo haizuii uhuru wa kuabudu. Aidha akafundisha kwamba, si haki kutumia upanga kwa mpinzani ambaye hana upanga na haya ndio maelekezo ya uislamu.
Shutuma za Abu Halima Kuhusu jambo hili zinaibuka tena kwenye ukurasa wa 7 ameandika
"Wakagundua kwamba mtu ambaye watampata kwa urahisi kwenye jambo hili ni Mirza Ghulam Ahmad ....." (ukurasa wa 7)
Mirza Ghulam Ahmad a.s hana shida hiyo kama adhanivyo Abu Halima , aliweza kukataa ushauri wa baba yake wa kumtafutia ajira Serikalini, na akamwambia kwamba nakushukuru baba, ila mimi ninae mwajiri wangu tayari, akimaanisha Allah ndiye mwajiri wake kwani Alishachagua kumtumikia Allah kwa kuutetea Uislamu.
Katika maisha yake yote ameishi kwa kuutetea uislamu dhidi ya maadui zake wakali. hususan Wakristo, Waarya, Masingasinga. Kazi hiyo adhiim aliifanya tangu hajapata cheo cha Imam Mahdi. Allah alimchagua ili aisimamie sheria ya Kiislamu katika nyakati hizi ambapo Waislamu wamejisahau, wamezama katika anasa za dunia na kuiacha dini katika ukiwa kama kwamba haina mwenyewe. Basi akasimama "Simba" wa Allah na maadui wote wakataharuki.
Atakuwaje kibaraka wa Waingereza wakati yeye ndiye aliyejasiri kuwalingania hadharani kwamba Yesu si Mungu na kwamba Yesu ameshafariki zamani Mungu hafi.

Abu Halima bila haya ameandika

Endelea Uk wa 8..

HATIMA YA WAPINZANI WAWILI WA SEYYIDNA AHMAD[AS]

(SH. MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII NA ABDULLAH ATHAM) KUSHINDWA KWA MAADUI

wanaochagua kuwapinga manabii wa Mungu bila shaka wanayo bahati mbya kwani Mwenyezi Mungu amesema kuwa:

Na hakika wamefanyiwa mzaha mitume wa kabla yako. Lakini yakawazinga wale waliofanya mzaha miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha. Sema safirini katika nchi, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wakadhibishawo. [6:11-12]

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad as alipata istshahada ya namna hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Moja wapo za funuo zake inasema "Nitamfedhesha kila anaetaka kukufedhehesha."

USHUHUDA WA SHEIKHE MUHAMMAD HUSSAIN WA BATALA.

Utukufu na heshima ya Hazrat Ahamad kwa wale waliomjua inaweza kupimwa katika maneno ya kiongozi na mwanachuoni mmoja wa kiislamu, ambae baadae alikuja kuwa mmoja wa maadui zake wakubwa; ambae kwa hakika, aliongoza uadui ambao ulikuwa mkubwa juu ya Masih alieahidiwa as na madai yake, mtu wa kwanza kutoa fatwa ya ukafiri kwa Masihi a.s, kiongozi huyu hakuwa tu mtu wa kawaida bali, Alikuwa ni sheikh mkuu alie kubaliwa katika madhehebu ya ahli hadith. Aliandika maoni yake juu ya barahiin Ahmadiyya, kitabu cha kwanza kikubwa cha Hazrat Mirza Ghulam Ahmad as. Katika gazeti lake la ishaa'at-us-sunnah, sheikh huyu aliandika akithibitisha ukweli wa Masih aliyeahidiwa a.s kwa kusema kwamba:

''Mtu awezae kufikiri kuwa tunatia chumvi kama tukisema kuwa tunamfahamu mtungaji wa kitabu hiki vizuri sana. Utakatifu na usafi wa tabia ya Seyyidna Ahmad as; ''mtungaji wa barahiin Ahmadiyya anajulikana sana kwetu. Kwa kweli, wachache tu wanajua zaidi juu ya fikara zake, juhudi yake n.k. kama tujuavyo sisi. Yeye ni mtu wa wilaya yetu, na alipokuwa mdogo alihudhuria mafunzo ya namna moja pamoja nasi. [tulisoma qutbi na sharah mulla pamoja]. Tangu siku zile tumekuwa tukiandikiana barua na kuzungumza mara kwa mara. [ishaa'at-us sunnah, 6;7].

hakika mfano wake katika zama hizi, na kwasababu ya haja za zama hizi zetu hakijajapatikana kitabu chochote kilicho mfano wa hiki katika taarikh nzima ya Uislamu. Juu Ya baadae hakuna awezaye kusema. ''Mwenyezi Mungu huenda akafunua jambo baada ya wakati huu. ''Ama juu ya mtungaji, tunaweza kusema ya kuwa kumekuwa na waislamu wachache, kama kulikuwa na wowote, ambao wameendelea kwa kudumu katika kazi ya islamu, kazi kwa mali na kalamu, kwa tabia njema na kwa maneno ya mdomo kama tunalaumiwa ati tunatia chumvi, hebu basi tuambiwe kwa uchache, kitabu kimoja tu kilicho andikwa zama hizi, ambacho kinajibu upinzani wa maadui wa Islamu, kama maarya na jamaa wa brahmu, kwa ngumvu ileile na juhud ileile. kadhalika tuambiwe juu ya masahibu wawili watatu tu ambao wameazimia kuutumikia Uislamu kwanjia kama hiihii, kwamali na kalamu na kwa maneno na nafsi; ambao maisha yao pia ni waqfu, ambao wanaweza kusimama kiume kuwaita maadui wa Islamu waje kushuhudia kazi hizo na kuondolewa na mashaka juu ya ufunuo kupatikana na ambao wamewafanya wasio waislamu waonje ukweli wa Islamu''(Ishaa'at-us-sunnah,jalada la 6 namba 7).

SHEIKH MUHAMMAD HUSSAIN BATALAWII ALIMPINGA HAZRAT MASIH MA'UD BAADA YA MADAI YAKE

Sheikh Muhammad Hussain wa Batala, badae alianzisha upinzani kwa madai ya seyyidna Ahmad as na kutumia maisha yake yote kwa kumuita kafiri na muongo Masih as. Kama makafiri wa makka ambao kabla ya madai ya

Mtukufu Mtume Muhammad saw walimuita mkweli na mwaminifu, na baadae walipitisha maisha yao katika kumkadhibisha.

Ama uadui na upinzani baada ya madai ya mtu hauwezi kuwa na maana sana, tunafahamishwa na Quran tukufu kwamba haiwezekani mtu awe ameonekena baada ya kujaribiwa sana, kuwa mwema na mkweli kwa rafiki na hata maadui zake, na ghafla ageuke na kuanza kuongopa juu ya Mwenyezi Mungu. Kama maisha ya mtu yamejulikana kuwa safi kabisa hata na maadui zake, Mwenyezi Mungu hatambadilisha mara moja kuwa mbaya wa wanadamu. Mtu anayesimama imara kabisa katika majaribio makubwa, na ambaye aachani na haki na hata aone hatari kubwa mno. Hawezi ghafla kuanza kuzua juu ya Mwenyezi Mungu. Haiwezekeni mtu kulipwa maovu kwa mema.

Wala Mwenyezi Mungu haufuti moyo wa mtu mwema na mkweli na kumjaza uwongo na udanganyifu. Mtume saw aliwaita maadui zake mara kwa mara na kuwataka wataje hata kosa kidogo katika mwendo wa kibinadamu ambao alipata kulifanya tangu hapo kabla. Je, hawakumuhesabu kama mbora wa wanadamu? Hakuna hata mmoja alie kubali wito huu. Hivyo hivyo, masihi aliyeahidiwa a.s alitangaza kwamba alihakikishiwa kwamba maadui zake hawataweza kutaja hata dhambi moja katika mwendo wake mzima (Nuzuul-ul-masih, uk 212).

Kwa kusaidiwa na uthibitisho huu aliwaita maadui zake mara kwa mara na kuwataka wataje hata dhambi ndogo tu aliopata kufanya kabla ya madai yake. Walimuona akiwa mtoto hata mtu mzima walimtambua kuwa mfano mwema kwa utawa wake. Basi aliwaita mara nyingi katika jambo hili. Wale ambao walimjua tangu utoto wake walikuwako. Waliweza kuwa wapinzani wake wakubwa, lakini hawakuweza kuficha ukweli juu ya tabia yake njema tangu zamani.

Seyyidna Ahmad as. Kwa mujibu wa ushuhuda wa ulimwengu, alikuwa mtu bora sana. Alikuwa mtawa sana kwa maoni ya wale walio mjua tangu zama za utoto wake, wengi wao wakiwa mabaniani, masinga singa na waislam. lakini hawathubutu kumtolea kosa maisha safi ingawa hawakuamini madai yake. Kwa ufupi utakatifu wa tabia ya mtu ni hoja yenye nguvu sana juu ya ukweli wa madai yoyote ya unabii. Hoja hii imetolewa na Quran juu ya

Mtume saw. Inaweza kutolewa pia kwaajili ya madai ya masih as. Ukweli wa madai yake unakubaliwa na utakatifu wa maisha yake kabla ya madai yake. Jambo hili hailikanwi na maadui zake. Hivyo basi, tabia ya seyyidna Ahmad as ni ushuhuda juu ya ukweli wa madai yake.

UTABIRI WA MASIH AS WATIMIA

Utabiri wa masih as unaosema kuwa Na nikaona kwamba mtu huyu aliniamini Imani yangu kabla ya kufa kwake, nikaona kwamba hakuna neno la takfiri na kutubu, na haya ndio maono yangu na matumaini kwamba Mola wangu ataifanya kweli, na Amani iwe juu yake anae fuata muongozo.

Utabiri huu uliweza kutimia kikamilifu kama utabiri ulivyo jieleza hapo juu, sasa mtu anaweza kujiuliza kuvipi Sheikh Muhammad Batalawii ambaye alikuwa adui mkubwa wa islam, je, anaweza akamkubali masih ma'ud as kweli na ikaonekana kidhahiri yeye (Muhammad husein) hakumkubali masih as mpaka akafariki. Lakini ikumbukwe kuwa hazrat Mtume saw aliota ndoto kwamba amemuona Abuu jahl peponi. Hapo hata Mtume saw hakuielewa ndoto hiyo lakini tunakuja kuona ndoto ilikuja kutimia kwa mwanae Hazrat Ikram ra ambaye alikuja kuukubali uwislamu siku ya ushindi wa islamu. Vivyo hivyo ndoto ya masih as ilikuja ikatimia kwa wanawe wawili wa Sheikh Muhammad Husein Batalawii ambao walikuja wakajaza baiati kwa mkono wa Hazrat Khalifatul Masih wa pili ra, na ndoto ikatimia kikamilifu (tadhkrat u.k 269)

KIFO CHA SHEIKH MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII

Kuhusiana na kifo cha sheikh Muhammad Husain batalawii yeye alikufa kifo cha kawaida tu katika enzi za khalifa wa pili wa masih as, mwaka 1920. lakini kutokana na laana nyingi ambazo alipata kutokana na kumfedhesha Masihi as na Masih as akaweza kutamka laana nyingi kwaajili yake, yeye baada ya

kufa aliweza kusahaulika kiasi kwamba hakuwa na wafuasi ilihali kabla hajafariki alikuwa na wafuasi wengi mno lakini mpaka sasa kaburi lake halijulikani na wala hakuna mtu anaye mfuatilia isipo kuwa waahamadiyya tu na hii ni kwasababu alikuwa mpinzani mkubwa wa masihi as. Na hii ni moja ya adhabu kubwa ya Mwenyezi Mungu ambayo aliipata baada ya kifo chake, na pia ni moja ya ishara ya ukweli wa Masihi as ambaye alikuwa anaonekana ni dhalili kiasi kikubwa ambaye baada yake Mwenyezi Mungu akainua kudra yake nyingine ya kuwaletea Imani wafuasi wa Masihi as (yaani ukhalifa) kama alivyoinua ukhalifa baada ya kifo cha Mtukufu Mtume saw na waislamu wakapata Amani kubwa na Islam ikasonga mbele kiasi hiki kwamba ujumbe ulifika ulimwengu mzima na vivyo hivyo ilivyotokea baada ya kifo cha masihi as. Na pia wafuasi wake mpaka leo huenda kuzuru maeneo matakatifu alipokuwa anaishi Masihi as na watu kuona kaburi lake mioyo hubadilika na uchamungu huzidi kiasi hiki kwamba mtu kueleza inakuwa ni muda isio hesabika.

Sasa anagalieni wenyewe kwamba mtu ambae alikuwa na wafuasi wengi na alikuwa imamu mkubwa, inakuwaje baada ya kifo chake asahaulike kiasi hiki kwamba hakufanya kazi yoyote na yule mtu ambaye alikuwa anaonekana dhalili mpaka sasa ujumbe wake unaonekana na unajulikana duniani kote na watu kila kukicha wanaendelea kujiunga katika dini yake kwa hakika hii ni fadhila ambayo Mwenyezi Mungu aliwaahidi watumishi wake watukufu kuwa watawashinda wapinzani wao hata kama wakifanya juhudi kiasi gani. Mwenyezi Mungu anasema katika kuran tukufu kuwa:

كَتَبَ ه اللَّ لَّغْلِبَ ه ن أَنَا وَرُسُلِي إ ه ن ه اللَّ قَوِيٌّ عَزِيز

''yaani Allah amekwisha andika: bila shaka nitashinda mimi na mitume wangu! Hakika Allah ni mwenye nguvu, mwenye ushindi kamili''. (58:22).

Kwahiyo kutokana na ahadi hii ya Mwenyezi Mungu kwaajili ya watumishi wake ikatimia kikamilifu.

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

DAKITARI KATUTOKA

Jina la Mola Maliki, Muumba Alotukuka.
Kwenye wake umiliki, kwa khushui najiweka.
Nitoe kilio hiki, juu ya Hamidu Jaka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Kijana wetu shafiki, dakitari msifika.
Asiyekuwa na chuki, na mchaji muafaka.
Ni pengo halizibiki, wala kusahaulika.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Hakuwa mtu fasiki, ni mwema wa kutajika.
Kwenye utii na haki, Jaka alijisimika.
Penye fujo na mikiki, pembeni alijiweka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Upole na urafiki, vilimjenga khuluka.
Hata alipohamaki, tabasamu lilitoka.
Kifo chake ni hilaki, taraji limetoweka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Khadimu kindakindaki, jamati alijitwika.
Kwa jaziba na ashiki, ujumbe alipeleka.
Kwa hoja za mantiki, wabishi aliwanyuka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Sala hakuitaliki, alidumu kuishika.
Kamwe nyuma hakubaki, adhana ilipotoka.
Imani na itifaki, kwake zilikamilka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Kujitolea malaki, kwa Mola hakujizuka.
Aligawanya riziki, kila ilipomfika.
Hakutaka unafiki, ubakhili kujivika.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Kwa wema alisabiki, kujitoa hakuchoka.
Huduma alishiriki, kwa bashasha akicheka.
Akatibu wenye dhiki, bila tozo kuwataka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Si ndwele zilomdhiki, hata akatuponyoka.
Ajali ya pikipiki, uhai imempoka.
Kifo hakiepukiki, ahadi ikishafika.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Huzuni haibebeki, subira yatuponyoka.
Kilio cha taharuki, cha kwikwi kimetushika.
Nyoyo zimevia maki, chozi latutiririka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Kazi ya Mungu ni haki, na si yenye kupingika.
Tuombe kwa sitahiki, sujudani kuanguka.
Apewe kwa tahakiki, pepo iliyotanuka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Nyuma yake walobaki, tuwaombee fanaka.
Mpaji Mola Razaki, awakinge na mashaka.
Utulivu na riziki, kwao visije punguka.
Dakitari katutoka, huzuni haibebeki.

Abu Talha, Abdullah Hamisi Mbanga
(Kungwi) Radio Ahmadiyya 99.3 Mtwara.

NI HISANI YAKE MUNGU, DINI KUITUMIKIA

Yu Pweke Kakamilia, Wa shani Mwenyezi Mungu
Kwa kwikwi namlilia, Dini Yake iwe yangu
Niweze Mtumikia, Awe radhi nami Mungu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Dini kuitumikia, ni hisani Yake Mungu,
Yeye Ndiye Huamua, wa kuchunga walimwengu
Ni ukweli asilia, wa kale tangu na tangu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Mitume huwateuwa, Mwenyewe Mwenyezi Mungu
Makini huwakagua, Cha mfinyanzi wa vyungu
Wahyi huwashushia, kuasa tamu na chungu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Sisi Katupendelea, katuondoa ukungu
Masihi kutujilia, na ishara za kimbingu
Fahamu katutilia, tumsaidie Mungu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Waqfu tulojitoa, sikizeni ndugu zangu
Na wote wa Jumuia, tulo mafungu mafungu
Tuzihalisishe nia, kumtumikia Mungu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Wapo mabilionea, wajawe Mwenyezi Mungu
Hazina walojazia, hebu waone wazungu
Juhudi wamezidia, lakini dhidi ya Mungu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Waqfu kujitolea, kwa nje kuna machungu
Ila ukivumilia, mwishowe uwe wa Mungu
Mola atakunyeshea, yenye neema mawingu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Waqfu kuuachia, wamkimbiaje Mungu?
Dunia waegemea, na hali ina mvungu
Huogopi kutokea, ukajuta ole wangu!
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Maombi ninarudia, nikubali Mola wangu
Niweze kutumikia, kwa yote maisha yangu,
Ukue na kuchanua, uimara ndani yangu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Na huu ndio wasia, nawaachia wanangu
Wasije wakabeua, kumtumikia Mungu
Wakaipotea njia, wakumbwe kizunguzungu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

Mwisho nikimalizia, nikiri unyonge wangu
Kimo sijakifikia, hata cha mduduchungu
Allah takabali dua, zifunguke zangu pingu
Ni hisani Yake Mungu, Dini kuitumikia.

SH. AME

DINI YA KISTAARABU

Usafi kipaumbele, kuoga piga mswaki
Harufu kuiondole, wenzo kero isibaki
Manukato uyatile, shombo kwako lisibaki
Dini ya kistaarabu,

Nguo nayo mavazile, usafi yaangalie
Lengo lake sipotele, sitara na uremboe
Vya Siri siviachile, hadhara vianikie
Dini ya kistaarabu,

Chakula kiheshimile, ukile umetulia
Mikonowo unawile, sile ujatawabia
Na Kiasi ukikule, taratibu Kwa hatua
Dini ya kistaarabu,

Salamu usalimile, kila mara kikutana
Chuki usiwa wekele, wenzio ukagombana
Zawadi uwagawile, mpate kukumbukana
Dini ya kistaarabu,

Ukweli uzungumzile, uwongo uukimbie
Haki uishuhudile, ukweli siufichie
Ushahidi utolile, usipange ukimbie
Dini ya kistaarabu,

Upendo dhihirishile, Wote wakukimbilie
Sio kuku Wala kwale, huruma uwapatie
Siwatese vile vile, kikuona wachukie
Dini ya kistaarabu,

Haki nayo adilile, ni kanuni ya Amani
Katu sidhulumulile, utakuwa vuruguni
Adilifu ushikile, mmoja sipendeleni
Dini ya kistaarabu,

Kiburi utukutule, viache na usogee
Nidhamu nawo upole, kama kutu ng'ng'anie
Heshima na ikuvele, uvivu uuachie
Dini ya kistaarabu,

Mungu muabidilile, na ibada ishikilie
Kibudu sijifilile, molawo simtambue
Dini kusaidilile, njia njema utambue
Dini kistaarabu.

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

MASIHI WAKE NABIA

1. Itazame sura yake,
   Shangaa na usichoke,
   Shani ya haiba yake,
   Masihi wake Nabia.

2. Sikiza kauli zake,
   Kina cha fasaha yake,
   Kamili yakini yake,
   Masihi wake Nabia.

3. Chunguza mwenendo wake,
   Uone upole wake,
   Tabu kupata mwenzake,
   Masihi wake Nabia.

4. Imba nae nyimbo zake,
   Uonje upendo wake,
   Ladha ya mizani yake,
   Masihi wake Nabia.

Mussa Mpinga
Dar Es Salaam

MOSHI MUHAMMAD MLEKYAKULE MSIMBE AMEAGA DUNIA

Kutoka Uk 01..

hakujitangaza kama Ahmadiyya kwa takribani miaka 9 au 10.

Akiwa katika shughuli za ufundi Seremala ambapo alijifunza kwa baba yangu mdogo marehemu Mzee Ally Selemani Malenge ambaye alikua shemeji yake, Karakana hiyo ya useremala alijiunga mwaka 1973 au 1974.

Katika karakana hiyo walikuwepo wafuatao Marehemu Baba yangu mzazi Mzee Juma seifu Sango aliyepata kuwa imam wa msikiti mkuu wa Nguruka kati pia Mzee Ally Selemani Malenge aliyepata kuwa Imam wa Msikiti.

Baada ya kujifunza kwa muda Mzee Moshi aliamua kuhamia Dar es salaam kwa lengo la kujifundisha dini kwani baada ya kua Ahmadiyya alijua upinzani mkubwa ambao atakutana nao hivyo akaona kuna umuhimu wa kujifundisha dini ili aweze kukabiliana na upinzani wowote utakao jitokeza. Huko Dar es salaam alikutana na Amir na Mbashiri mkuu wa wakati huo Maulana Jamil Rahman Rafiq Mzee Moshi alifanya kazi ya kuuza vitabu na alijifundisha dini. Baada ya muda Mzee Moshi aliamua kurejea Nguruka ambapo mara baada ya kufika alianza harakati za mahubiri kwa kasi kitu ambacho kiliwachukiza sana Masheikh na mwisho wa siku akatangazwa kwamba yeye ni kafiri na akifa asizikwe kwenye makaburi ya Waislaam, na waislaam wenye maduka wasimuuzie bidhaa. Pia alinyang'anywa mke na alibaki na watoto watatu akiwalea mwenyewe. Kunyanganywa mke haikumrudisha nyuma bali aliendelea mbele kwa mapambano.

Baada ya Jamaat kuongezeka mwaka 1991 Mzee Moshi aliamua kuitoa nyumba yake aliyo kua akiishi na familia yake kua Msikiti na yeye akaenda kupanga. Hii ndio ilikuwa hali yake katika kujitolea.

Aliporudi Nguruka hapo ndipo juhudi ya kuhubiri na mapenzi yake kwa Ahmadiyya alipo ya dhihirisha. Baada hupambana na upinzani mkubwa na kuto yumba likiwemo suala la kunyang'anywa mke kua akitaka kuishi naye asilimu kana kwamba sio muislam (wakati ule suala la kuoa au kuolewa nje ya jamaat lilikua halijatiliwa mkazo kama hivi sasa).

Ajabu ya masheikh wa kisuni wakati wanamfungisha ndoa ya kiislam alikua ni Ahmadiyya na walikua wanajua vema kwamba mtu huyu ni Ahmadiyya. Wao walidhani labda kwa kumnyang'anya mke wangefanikiwa kumtoa katika Ahmadiyya na kuacha harakati zake za kuihubiri Islaam Ahmadiyya. Lakini kinyume chake Mzee Moshi hakutetereka wala kuyumbishwa na yeyote bali alishikilia msimamo wake na mwisho wa siku akanyang'anywa mke kwa sababu tu yeye ni mfuasi wa Masihi aliye ahidiwa.

Katika uwanja wa siasa nakumbuka tukio kubwa lililotokea hadharani shule ya sekondari Nguruka ilipo kua inajengwa baadhi ya michango ilichangishwa kwa risiti zisizo na kopi hivyo kuhatarisha fedha kufika sehemu husika kwa usahihi, Mzee Moshi Mohamedi aliwaambia wananchi wasilipe michango mpaka wapate risiti shataki. Habari ya Mzee Moshi kuwashawishi Wananchi kugomea michango ilifika kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma wakati huo alikua mzee Yusuf Makamba, akiwa katika mkutano wa hadhara ambao mimi nilihudhuria Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mzee Yusufu Makamba akauliza kwa ukali nani kazuia wananchi kuchangia sekondari

Mzee Moshi bila uwoga alisimama na kujibu ni mimi hapa Mkuu wa mkoa akamwambia kaa. Utaona ni kwa kiasi gani aliweza kusimamia haki bila uwoga.

Pia akiwa katika siasa huko alibahatika kumpatia video za Mihadhara ya Ahmadiyya Mbunge wa wakati huo Kigoma kusini Mheshimiwa Kifu Gulamu Hussein Kifu 2000 – 2023 Mheshimiwa Mbunge alivyoona jinsi Masheikh wa kisuni wanavyo shindwa kujibu hoja za Ahmadiyya na kushindwa na Masheikh wa Ahmadiyya Mbunge huyo hakuamini kama ni kweli Masheikh hao wameshindwa bali inawezekana wakawa ni Ahmadiyya watupu wanafanya maigizo tu, hivyo akataka aone mwenyewe kama Suni wanaweza kushindwa kirahisi hivyo.

Ni kweli kwa msaada mkubwa wa Allah mjadala uliandaliwa Mbunge aliwaita Masheikh ambao aliamini kwamba ni wajuzi wa dini walio bobea na upande wa Ahmadiyya Walileta Masheikh wao, Mjadala ulifanyika na matokeo yake Masheikh wa Kisuni walishindwa vibaya. Unaweza kuona mjadala huo katika YOUTUBE kwa kuandika mjadala wa Nguruka AHMADIYYA VS SUNI NGURUKA. Kufanyika kwa mjadala huu yalikua ni matokeo ya juhudi kubwa za Mahubiri ya Mzee Moshi.

Watu wengi hunuliza nini kilitokea baada ya mjadala je? Mbunge alisema nini? Ni vema nijibu kwa maneno ya masih aliye ahidiwa Hadharat Mirza Ghulam Ahmad kwa faida ya wote walio hudhuria au kufuatilia mjadala huo alisema "Ishara moja yatosha kama moyoni mwa mtu mnauchamungu"

Mambo aliyofanya Mzee Moshi Muhammad ni mengi naweza kusema maisha yake yalikua mahubiri sidhani kama kuna siku yeyote maishani mwetu tulikutana naye bila kujadili Ahmadiyya.

Siku moja tulikwenda katika kanisa la Pentekoste Majengo Nguruka, Bweru baada Mkristo mmoja aliyedai alikua mwislam sasa kaokoka lakini akiwa mwislam alisoma LIBYA na kupata PHD hivyo anafahamu vizuri Islamu si Dini ya kweli Jina lake alikua anaitwa HAMISI PAULO Tukiwa wawili tuliomba kanisani hapo tufanye nae mjada Bw. HAMISI PAULO aliogopa,

Watu wengi wanaishia kusema unabii umeisha lakini hajui kazi ya Nabii, ili kujua kazi ya Nabii angalia maisha ya wafuasi wake kabla Nabii hajafika na baada ya Nabii kufika au waliomkubali baadae ilikuaje hali yao kabla na baadaye.

Hivyo tuangaliapo maisha ya mzee Moshi Muhammad sahib, hakupata Elimu rasmi ya dini au ya dunia alisoma kidogo sana, Lakini baada ya kumkubalia Nabii wa Mungu ambaye pia ajapo huipa mioyo ya binadamu shauku kubwa ya kujitolea bila kukata tama au kuhisi mbona Fulani hajitolei mimi pia niache.

Licha ya Mzee Moshi kunyang'anywa mke na mashekh yeye aliwanyang'anya Islam ya kweli yenye kuweza kuhubiri na kuwaita wasio Waislam kwenye njia iliyo nyooka ambayo ni Islaam ya kweli Islam Ahmadiyya; aliwaambia hakuna majini wanao wakamata watu au kuwaingia kichwani kina mama na kupagawa pia uchawi si kitu kinachoweza kubadili uhalisia wa kitu mtu ambaye hakusoma akaitwa Mw.sheikh ni kwa sababu Baraka za unabii,

Wapo watu ambao wameanza kuwa na fikra ambaozo sio sahihi kuwa Moshi amefariki Ahmadiyya itakufa Nguruka mimi naamini kwa msaada wa mwenyezi Mungu Moshi umeondo sasa utakuja moto.

Yeye kama nilivyo sema hakusoma laki alivyo hubiri kwa kua ni kazi ya Mungu aliwapata wenye Elimu wajuao kusoma Qur'an lugha ya kiarabu sasa Jmuiyya ya Nguruka ina watu wenye elimu kubwa ya dini kuliko Mzee, Naamini kwa msaada wa mwenyezi Mungu Ahmadiyya NGURUKA itaendelea kuimarika na kukua kwani inawatu mahiri na wenye kiu ya kujitolea kwa ajili ya dini hakika Mzee Moshi ameondoka lakini ameacha kizazi ambacho ni imara kitakacho endeleza kwa juhudi kubwa yale aliyo kuwa akiyafanya.

Mwito wangu kwa sisi tuliobaki tukielekea kutimiza miaka 100 ya jamaat Ahmadiyya Tanzania tuwe wabunifu zaidi katika mahubiri yetu tukitumia mabango ya kisasa vipaza sauti matangazo ya tukio husika n.k Pia kupitia kitabu Sheria ya kutunga mashauri kilicho andikwa na sheikh kaluta Amri Abed Mzee Msoshi Muhammad alijifunza mashairi kutunga na pia kughani shairi aliloghani sana katika mikutano ya jamaati ni wamchao Rahman ndio wenye mwisho mwema

Pia shairi jingine alopenda kuimba KINDA NINGALI MTINI SINA WA

KUNILEA

1). Baada ya Moshi kutoka
Ruhusu moto kuwaka
Isaidie Nguruka
Msifika ewe Mola

2). Kwa zako hasa baraka
Jamati na sasa shika
Isipate tetezeka
Bali ipate imara

3). Nasiku zitafika
Nanyoyo takumbuka
Mbali sasa wamefika
Naujumbe wa masihi

4). Twakuomba kwa hakika
Moshi apate sitirika
Yale aloghafilika
Eemola msamehe

5). Hakuna Alokamilika
Naya Dunia mashaka
Kwa yako rehema shuka
kumfunika twaomba

6). kituoni nimefika
machozi yananitoka
alikua kwa ngufika
rafiki wa kupendana.

Baadhi ya watu katika Jamaat Ahmadiyya walidhani mzee Moshi Muhammad alikua ndugu yangu wa damu pia hali hii pia ilitokea mbagala Dar es salaam kizuiani tuliko kua tukiishi pia Nguruka. Watu walipata kumuuliza hata baadhi ya ndugu wa damu wa Mzee Moshi tena wengine walimuuliza mbele yangu, kumbe ulikuwa ni undugu uliofunganishwa na Nabii kutoka India.

katika harakati zake za Mahubiri Mzee Moshi Muhammad Mlekeyakule alikutana na vitisho toka kwa masheikh wa kusuni ambao walimtishia hadharani kuwa kama hataacha kuhubiri Ahamadiyya lazima watamroga kwa kawaida sisi Ahmadiyya hatuamini kuwa uchawi unaweza kubadilisha uhalisia wa jambo hivyo mzee Moshi katika kipindi hicho aliomba ili mungu ampe umri mrefu ili isije ikitokea aje waliomtishia wapate kujisifu bila ukweli wowote na ndivyo ilivyotekea ameishi toka miaka ya 80 mpaka kufariki tar 07/06/2025. Walimwambia hawezi kufanikiwa katika mahubiri yake kwa sababu hana elimu ya dini na pia waahmadiyya ni makafiri. Lakini leo hii Mzee Moshi anaiaga dunia akiwa ameacha kundi kubwa la waumini tena wengine wakiwa ni wasomi wabobezi wa dini.

Akiwa katika uwanja huo wa mahubiri ambao hakupata hata siku moja kusita kuhubiria alipambana na mzee mmoja mwenye asili ya Ujiji Alhaji Kintu Shomari ambaye alikua mpinzani wa jamaat Ahmadiyya akamwambia wewe Moshi huna elimu ya dini unawezaje kuhubiri, Ndipo walipo kubaliana wasome hadharani maneno ya kuanzia kutawadha na sala kwa kiarabu na tafsiri yake kwa Kiswahili katika mashindano hayo Sheikh wa ujiji hakutokea.

Neno letu la Mwisho sifa zote njema zinamuhusu Allah.

MAANDAZI YA KUOKA

MAHITAJI YA MAANDAZI

°Ngano vikombe 3
°Baking powder 1/4 kijiko cha chai
°Siagi vikiko 2 vya mchuzi
°Vanilla kijiko 1 cha chai
°Hamira ya chenga kijiko 1 chai
°Chumvi 1/4 kijiko chai
°Sukari kijiko cha mchuzi 1 1/4
°Maji ya uvugu vugu kiasi



KUANDAA NA NA KUOKA

1 :Tia unga katika beseni kisha tia hamira, baking powder,chumvi, sukari, vanilla, na siagi kisha changanya unga wako vizuri.

2 : Baada ya hapo tia maji kidogo kidogo na anza kuponda unga wako ponda kwa dakika 3 ila usiulainishe saana.

3 :Acha Kwa dakika kadhaa kisha kata na achatena kidogo. ..lambisha mafuta katika chopmbo cha bati kisha panga maandazi yako na lambisha mafuta juu ya maandazi na tia katika oven kwa muda mchache maandazi yako yatakua tayari kuliwa.

MAJIBU KWA MASALAFI

Kutoka 04

" Kwa hivyo ukadiani ni harakati zilizoundwa na Uinegerza kwa ajili ya kupingana na Uislamu " (Uk . 9)

Lakini hajui Abu Halima kwamba sisi na wao tumewekwa katika kapu moja, hebu soma maneno haya:

"Madhehebu mengine yaliyoanzishwa na Ukoloni wa Mwingireza sambamba na ukadiani, ni pamoja na Ubahai na Uwahabi"

Rejea kitabu (UPOTOFU WA MADHEHEBU YA UWAHABI Uk .40)

Toleo la nne (2020)

Nitatoa maelezo zaidi mwishoni mwa makala hii kuhusu UWAHABI ambao ndio USALAFI, ANSWAR SUNNA n.k

SURA YA SITA

MTUME WA MWISHO NI NANI?

Abu Halima ameandika :

"Makadiani wanaitakidi kwamba mlango wa Utume bado haujafungwa" .

(ukurasa wa 12)

Ni kweli, tunaamini hivyo na kama Abu Halima anaitakidi kuwa Utume umefungwa atuambie umefungwa na nani? wapi? kwenye Qur-ani au hadithi?

Abu Halima na mashekhe wake hawaisomi Kur-ani, angekuwa anaisoma angeikuta aya hii .

"HUWATEREMSHA MALAIKA KWA AMRI YAKE WAKIWA NA WAHYI KWA YOYOTE AMTAKAYE MIONGONI MWA WATUMISHI WAKE AKISEMA: ONENI KWAMBA HAKUNA MUNGU ISIPOKUWA MIMI , KWA HIVYO NICHENI MIMI TU"

(Sura Annahl, 16 : 3)

Allah Ametamka maneno:

" *YUNAZZILUL – MALAAIKATA BIRRUUKHI*" yakiwa ni kitendo kinachoendelea, yaani (fi'lu mudhwari) na hii Kur-ani ndicho kitabu cha mwisho cha sheria kinaendeleza utume, hakijafunga . Je Abu Halima ameona wapi utume umefungwa?

Hata Mtume[saw] hana habari ya kufungwa utume maana alishatuagiza kwamba atakuja Isa mwana wa Maryam akiwa ndie Imam Mahdi naye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kama nilivyobainisha katika sura ya nne.

Kwa kumsaidia Abu Halima pamoja na wasomaji wetu, ni kwamba Utume uliokoma ni ule wa kuleta sheria tu, kwani Kurani ndio sheria ya mwisho. Lakini Mitume wa kuja kuisimamia sheria aliyoileta Mtume[saw] wataendelea kufika. Haya hatuyasemi sisi Waahmadiyya tu bali yameshasemwa na wanachuoni kadhaa, kama vile

1. Sheikh Muhiddin Ibn Arabi [RH a] amesema :

"Utume uliokatika kwa kufika Mtume Muhammad s.a.w ni utume wa sheria, sio cheo cha Utume"

Rejea: (Futuhaat Makiyya j.2 uk 3) Akasema tena yeye huyo Sheikh Muhuddin Rh. A : "Utume unaendelea mpaka siku ya kiama katika viumbe, ingawa (utume) wa kuleta sheria umekatika" Rejea (Futuhaat Makiyya j.2 uk 95)

2. Imam Abdul – Wahhab Sha'rani[Rh.a]

Ameandika: "Utume haukufungwa kabisa, Mtume ambaye hawezi kuja ni wakuleta sheria" Rejea: (Al-Yawaaqiit Wal – Jawaahir j2 uk . 39)

Wako wengi wenye maoni hayo kwa kutaja wachache:-

Hadhrat Abdul- Karim Jilani[Rh.A]

Hadhrat Mughira Ibn Shu'ba[r. A]

Mama wa Waaminio Aisha[r.a]

Sheikh Muhammad Kasim Nanutwi Rh .a na wengineo .

KHATAMAN NABIYYIIN NA LAA NABIYYA BA'DI

Ameandika Abu Halima :

"Wakapotosha maana ya hadithi ya Mtume[saw] inayosema :

Hakika hakuna Nabii baada yangu na pia wamepotosha kauli ya Allah isemayo :

Walaakin Rasuula llah Wakhaataman Nabiyyin . Yaani Bali ni Mtume na ni mwisho wa Manabii." (uk . 12)

Tatizo ni uchache wa elimu tu , au kung'ang'ania mazoea hata kama ni ya kijinga . Ebu tumsikie mama Aisha ambaye Mtume[saw] ametwambia tuchukue nusu ya elimu kutoka kwake .

Yeye anasema

" Semeni yeye ni khataman Nabiyyin lakini msimseme hakuna Nabii baada yake "

Rejea (Tafsiri Durrul-Manthur j.5 uk 204)

Miongoni mwa wanachuoni ni Imam Ali Al-Qari Rh. A yeye amesema :

" Khaataman – Nabiyyin maana yake ni kwamba , hatakuja baada ya Mtume[saw] atakayevunja sheria yake , na atakayekuwa mfuasi wake"

Rejea : (Maudhu'at Kabir)

Na mwanachuoni mwengine ni Seyyid Abdul- Karim Jilani Rh . a yeye amesema

" Hukmu ya unabii wa sheria imekatika baada ya Mtume[saw] hivyo amekuwa khaatama - Nabiyyin

" Rejea (Al – Insaanul Kaamil ml.36) Naye imamu Muhammad Tahir amesema

" Muradi wa LAA NABIYYA BAA'DI ni kuwa hatakuja Nabii wa kuvunja sheria yake "

Rejea : (Takmil Majma'ul Bihar uk 85)

Kwa hivyo imeeleweka kwamba sio Waahmadiya pekee wenye itikadi ya kuwa Mtume Muhammad[saw] ni wa mwisho kwa kuleta sheria .

***Itaendelea* SURA YA SABA**
toleo lijalo Inshallah

TABASAMU LA KWELI LA DR. HAMIDU SHAABANI JAKA SAHIB

Na Mahmood Hamsin Mubiru

ni bahti kukusanyika katika maisha ya mtu mmoja, ndipo tunapata taswira ya bingwa mpole na mwenye heshima, Dr. Hamidu Shaabani Jaka Sahib aliyefariki mjini Dodoma tarehe 06/08/2025 na kuzikwa na umati wa watu tarehe 07/08/2025 katika makaburi ya Wailes Temeke jijini Dar es salaam. “Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Tutarejea”

Dr. Hamidu Shaabani Jaka, kitinda mimba katika familia ya Bw. Shaabani Ramadhani Jaka yenye Watoto 7. Alizaliwa katika Kijiji cha Mfumbwe kata ya Mkuyuni Mkoani Morogoro Vijijini mwaka 1985. Alipata elimu yake ya msingi shule ya Msingi Songea. Kutoka hapo alikwenda shule ya Sekondari Usagara mjini Tanga na kidato cha tano na cha sita alikuwa shule ya Ufundi mjini Moshi. Baada ya masomo yake alijiunga na chuo cha tiba maarufu kama IMTU jijini Dar es salaam ambako alipata shahada yake ya kwanza ya Udaktari.

Toka udogo wake alikuwa mpole ambae wakati wote alibeba tabasamu. Hii ni sifa kubwa ya kwanza kuwa Daktari. Dawa ya kwanza ya mgonjwa ni tabasamu kwenye uso wa Daktari na tabasamu hilo alikuwa nalo Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib. Sifa yake ya pili ni kuelewa kuwa tiba hasa ni kutoka kwa Allah, na hivyo ni muhimu kumuomba ili Akuwezeshe kutoa tiba inayofaa. Tabasamu na kumtegemea Allah kulileta mafanikio makubwa kwa Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib ambaye alijali sana wagonjwa. Kwa kuonesha kujali kwake na bila kuonesha uchovu wa aina yoyote Bw. Nassir Matola alikuwa na tatizo la kiafya na alilifikisha kwa Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib ambae alimpatia dawa na jioni Kwenda kwake kuona mgonjwa wake anavyoendelea. Wapo baadhi ya wagonjwa ambao aliwasaidia kutoka mfukoni mwake waende kununua dawa.

Wafanyakazi wenzie wanamkumbuka kwa bidi kazini na kuwaheshimu wote. Risala iliyosomwa na Wafanyakazi wenzie ilitimiza ile shabaha aliyoitajwa Khalifatul Masih-II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) kwamba Ahmadiyya popote alipo yeye ni Balozi wa Islam ya kweli ambayo ni Ahmadiyya.

Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib hakuridhika na elimu aliyokuwa nayo katika fani ya Udaktari bali alienda kupata elimu ya juu zaidi katika Chuo Kikuu cha tiba cha Muhimbili. Masomo yaliyompa haki ya kuitwa Daktari bingwa.

Kwenye mkutano wa mwaka maarufu Jalsa Salana, alitumia wakati wake wote kuwatumikia wageni wa Masihi (as). Kazi hii alifanya kwa bidii na heshima kubwa. Bila shaka kuchaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Madaktari wa Kiahmadiyya ili ni kutambua mchango wake wa kutumia elimu yake ili kuitumikia Jamaat.

Elimu ina desturi ya kujenga kibri na kutowajali wale ambao hawakubahatika kama wewe. Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib hakuwa na majivuno ya aina yoyote. Aliendelea kuwaheshimu watu wote na ilitakiwa mtu mwingine kukueleza kwamba Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib ana elimu ya juu. Mwenendo huu unapatikana kwa Wanajamaat wa Ahmadiyya ambao huweka pembeni vyeti vyao na heshima zao ili kujitolea kufanya kazi ya Allah kwa kutumikia viumbe wake.

Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib aliwajali sana wazazi wake. Siku moja alifika kwa kaka yake Sudi Shaabani Jaka sahib, na kumwambia kuwa baba alikuwa anaumwa. Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib alisema, hakuna kupumzika hapa na wakafunga safari hadi nyumbani ambapo alimjulia hali baba na kumpeleka kwenye matibabu. Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib hakuwasaidia wazazi wake tu. Zipo similizi nilizozipata zinazoeleza ya kuwa Daktari alikuwa na mkono wa kutoa. Nakumbuka pia kupata mchango wake wakati nakwenda mtamboni kuchapisha kitabu cha; “Ahmadiyya na Ukombozi wa Tanzania”

Maisha ya Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib yanatufundisha Kutenda mema kwa viumbe wa Allah, kwani kwa kufanya hivyo unajihakikishia kukumbukwa kwa wema. Wanajamaat na wasio Wanajamaat niliozungumza nao walimkumbuka kwa wema Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib na wengine wakibubujikwa na machozi na kwa hakika jina jema haliozi.

Utafutaji wa elimu ni agizo la muhimu kwa kila Muislam. Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib hakuwa na mchezo katika utafuta elimu. Alionesha bidii na kuweka nidhamu katika kusoma. Nakumbuka pia nilipokuwa Katibu wa Elimu wa Jamaat, wanafunzi wa Jamaat walikuwa wanahitaji vitabu vinavyotakiwa mashuleni, na Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib alitoa mchango katika kununua vitabu hivyo.

Maisha haya ni mchezo na upuuzi. Kutokubali kutekwa na Dunia ingawa nafasi unayo ni jambo linalotupa fursa ya kutafakari. Wema hasa ni pale ambapo unaweza lakini unajizuia kwa ajili ya Allah.

Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib alikuwa kijana mbichi na vishawishi vyote vinavyowakumba vijana vilikuwa mbele yake. Kwa msaada wa Allah alivuka vizingiti vyote hivyo na hakuna uvumi wowote wa hovyo unaonathibishwa na jina lake. Kuogelea hadi ukafika Pwani katika Bahari hii iliyochafuka ambayo sisi tunaita maisha ni mafanikio makubwa sana. Wengi wameliwa na papa na majina yao yanapotajwa ni aibu na fedheha.

Kila alipokwenda aliweka wazi kuwa yeye ni Ahmadiyya. Tena si wa maneno bali wa matendo, bila shaka hakuna jambo la muhimu kwa hivi leo kuliko kuwa Ahmadiyya wa vitendo. Kwa hivi sasa tunao Waahmadiyya wengi ambao wamezaliwa katika Ahmadiyya. Jambo hili ni neema na lina hasara zake. Unapozaliwa katika Jamaat kama hukuzingatia shabaha ya kuanzishwa kwa Jamaat, kuwa kwako Ahmadiyya hakuleti mabadiliko yoyote. Dunia inatakiwa itoe Ushahidi kuwa wewe ni mtu tofauti kabisa. Watakukebehi wewe ni Ahmadiyya, lakini pembeni watatangaza yule bwana au bibi ukikutana nae ni ‘Assalaam Alaikum’, majirani zake wanampenda hana bughudha nao, ukibishana nae anajibu kwa upole na heshima na huku akitumia Qur’an Tukufu, Sunna na Hadithi. Tusi halimtoki hata kidogo mdomoni, penye uchafu wa aina yoyote humkuti, tena ukitaka kumuuzi umuambie mambo ya hirizi na Kwenda kwa waganga. Humsikii kukashifu dini za wengine. Huko ndiko kuwa Balozi wa Ahmadiyya. Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib alijitahidi sana kuweka bayana taswira hii ya Ahmadiyya kwa vitendo. Na siri yake kubwa ni kuvisoma vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) na kutokosa kusikiliza hotuba ya Khalifa Mtukufu inayotolewa kila Ijumaa. Ukitaka kuhuisha Imani yako jitahidi kusikiliza hotuba za Ijumaa za Khalifa Mtukufu na vipindi vingine vinavyorushwa na MTA.

Kifo cha Dr. Hamidu Shaabani Jaka sahib kimetukumbusha kwa mara nyingine kuwa daima tuwe tayari, kwani hatujui siku, saa au wakati wa kuondoka katika Dunia hii. Kama elimu hiyo hatukupewa kwanini tunaghafirika wakati tunajua kuwa safari hiyo ipo. Vipo vitu vingi ambavyo kila siku vinatukumbusha kuhusu safari ile. Hakuna miongoni mwetu ambaye hajawahi kufiwa. Huu ni ukumbusho tosha. Jua kila siku linachomoza na kuzama. Kuna somo ndani yake. Unalala unaamka zote hizo ni taarifa. Kama kuna kuna jambo lolote la wema tusisubiri kesho au kesho kutwa. Tufanye sasa hivi tena kwa haraka. Tusighafirike na ukumbusho mkubwa ni kusoma Qur’an Tukufu kila siku. Pilikapilika za ulimwengu huu zinaweza kutusahaulisha madhumuni ya kuja kwetu huku. Tusipoteze wakati. Shakespear ambae alisomwa sana na Hadhrat Khalifatul Masih-I, Hadhrat Maulvi Hakeem Nurdin (ra), aliwahi kusema; “Nilipoteza muda, sasa muda unanipoteza mimi”. Tukumbuke. Tuwe tayari. Na daima tuwe na masurufu yetu kibindoni. Hakuna masurufu bora kuliko Taqwa.

Allah mwenye uwezo wote mghofirie mja wako na mpatie mahala palipo pema.

Na neno letu la mwisho; ‘Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa Ulimwengu wote’.



SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka Uk.12

ambaye ni shekh alikuwa apande treni ya saa tano usiku kuelekea sehemu nyingine itakayomchukua masaa mengi mno kufika, treni hiyo ni ya vitanda tupu humo unaingia unalala mashine inaanza kutembea.

Safari ya Qadian ndio ilikuwa inafuatia kuanzia Delhi mpaka Amratsar kwa treni kisha kupokelewa kuelekea Qadian kwa gari, ni safari ambayo ingechukua masaa nane mpaka kumi, asubuhi tulijiandaa na safari ikaanza baada ya adhuhuru, Amiri wa Delhi alituaga na kutupa usafiri wake kutupeleka stasheni ya reli.

Watu wa India wanaendesha magari makubwa na mazuri na yakifahari mno, uwepo wa viwanda vya Tata na Mahindra na vinginevyo umewafaa sana watu wa India, na Suzuki india ni nyingi mno, hata tekenoligia ya magari yanayotumia gesi na umeme na bajaji zinazotumia umeme ni nyingi mno. Mabasi ya mwendo kasi yatumiayo umeme yanapita barabarani kwa wingi na ndio usafiri wa kawaida wa watu, mengine ni makuu kuu inayokuambia kuwa walianza mda mrefu kuyatumia na yote mtengenezaji ni Tata, sasa naona uwepo wa nyenzo hizi za usafiri na wingi wa watu kunaleta foleni mno barabarani na uendesheji wao wa kutojali utaalamu bali breki na honi na klachi kunaweka roho juu kwa watu ambao ni wageni wa hali hizi. Ni kawaida kuona magari yaliyoandikwa blow horn yaani 'piga honi' kwa nyuma, inapofika wakati magari yamekwama hayaendi kutokana na foleni wimbo unakuwa ni honi za ala mbali mbali, inaudhi ila mwishoe inachekesha.

Tulipopokelewa uwanja wa ndege wa Indra Gandhi Int. Airport moja ya uwanja mkubwa wa ndege niliowahi kutembea, na kupokelewa na wenyeji wetu na kupanda katika teki kuelekea markaz Delhi, binafsi namna ya uendeshaji wa dereva wetu sikuweza kulala, jamaa alikuwa cha kwanza anatafuna vitu Fulani alafu anatoka jasho sana, pembeni ana tambaa la kufutia jasho, na akitaka kutema mate anafungua mlango tungali tukuwa kwenye mwendo na kutema nje, loh! Mimi utulivu ulinitoka kabisa, na jinsi anavyokua anakata magari mengine barabarani ghafla ghafla, Ah wapi usingizi haukunijia kamwe.

Sikuwahi kuwasimulia wenzangu mpaka tuliporudi kwenye safari ya kutoka Jama Masjid kwani wote kwa pamoja tuliona viroja, dereva wetu wa bajaji alikuwa ameacha siti yake na kukaa katika chuma za pembeni huku akiendesha, lakini huku akijibishana na dereva mwenzie upande mwingine wakicheka kwa pamoja, sehemu ya foleni anashuka chini na kupiga soga na wenziwe. Mara tunaona dereva ambaye anaendesha bajaji huku amekunja nne mkono mmoja mfukoni huku anaendesha kwa mkono mmoja na sio kwa mwendo wa taratibu bali mbio na kushika breki za ghafla na madaha, lakini hapo hujaona ambaye anaendesha bajaji huku anaangalia filamu mtandaoni, nilipowasimulia wenzangu niliyoyaona kwa dereva aliyetuchukua kutoka uwanja wa ndege kila mtu alikuwa na jambo la kusimulia kuhusu uendeshaji wa magari na piki piki hasa katika mji wa Delhi.

Basi tulipoanza safari yetu kuekea stesheni ya reli tulipitia upande wa barabara za New Delhi na tukaanza kupata taswira nyingine na mji wote wa Delhi, kwani msikiti wa Jamaat upo upande wa delhi ya zamani (purana Delhi) ambako ukipita barabara zake utaona uchafu wa kila aina, ng'ombe na majibwa yakitembea barabarani huru, wanasema Serikali iliyopo madarakani inalinda mno uhuru wa ng'ombe na majibwa kusambaa mtaani bila kubughudhiwa, na ukionekana unaenda kinyume basi upo hatarini, sawa na tamaduni za kihindu ng'ombe ni kiumbe kitakatifu na alama ya dini yao, mwenyewe wanawatupia vyakula kando ya barabara kila siku, nao ngo'mbe wanakula na mbwa hivyo hivyo wanaishi na kuzaana bila shida. Hivyo basi tulivyopita New Delhi tukawa tunataniana kuwa hii ndio dehli ya kuwaleta familia na kupanga nyumba ya kuishi na sio ile ya ng'ombe na mbwa. Tulipokuwa tunakaribia stesheni tukakutana na foleni ya hatari ambayo taa ikiwaka gari linasogea sentimita kadhaa mara taa nyekundu imewaka, mara kuna anayegeuza arudi nyuma na wengine wanapitia ubavuni wengine wamekata tamaa tu vishoka wanawashushia mabegi na kuwabebea waweze kuwahi treni. Lakini dereva wetu alitupoza na kutuambia hamna shida tutafika kabla ya muda na kuwahi usafiri.

Kutokana na ukubwa wa India usafiri wa reli unategemewa mno, hivyo stesheni kujaa watu, vikumbo, msukumano na kuchanganyikiwa ni jambo la kawaida sawa na presha ya eneo husika na kila mikusanyiko hii huwa wenyewe wanatoa matangazo ya kuwa makini kuwa na vifaa vyako usije ukaibiwa yalikuwa yanaendelea, muda ulifika tukapanda treni katika behewa zuri lenye AC na vyoo na huduma zote na kuanza safari. India wanazo treni za tekenolia zote kuanzia za mwendo kasi za umeme na dizeli mpaka za mfumo wa kawaida. Behewa lilikuwa na siti za kutazamana na siti za kawaida za tatu kulia mbili kushoto. Tulikaa katika mstari mmoja wawili walikaa upande mmoja na wawili tukaa upande wa kulia, bahati yangu mbaya Yule wa tano wetu alikuwa mwanadada na alikuwa amekaa kushoto kwangu kwenye dirisha kabisa, kwa kumtazama tu alikuwa tayari ametaharuki kwa kukaa na sisi katika siti moja, alikuwa hataki kuwa huru mara aliniambia niangalie nafasi yangu nisimguse, mpaka alimuita mhudumu ambadilishie sehemu ya kukaa. Mimi nilitulia na kuangalia mchezo unaishia wapi, shida ni kwamba vyakula, maji, chai na huduma zengine zikija ni lazima zipitie kwangu ili zimfikie yeye , na hapo ndipo alibadili taswira na msimamo kwa sababu sikumuonyesha lolote isipokuwa kumhudumia tu na kumpa heshima yote. Mwishoni akaanza kuwa huru lakini kutoka na haya aliinuka na kukaa sehemu nyingine kwani nadhani nafsi ilikuwa inamsuta kwa kuhamaki kabla ya kujua amekaa na kina nani.

Tuliondoka jioni delhi nilichokuwa nakiona nje ni taa za mapambo tu kwani ilikuwa ni msimu wa sikukuu yao ya Diwali hivyo kumbi na majumba yote yalikuwa yamepambwa kwa taa kama tunavyoziona wakati wa Jalsa salana katika majengo ya Qadian, na kitu kingine ni ardhi ambayo kuanzia delhi mpaka Punjab ardhi yote imelimwa na hakuna hata pori, huku shamba lipo katika matumizi mwaka mzima, ukitoka mpunga ni ngano, ngano mpunga au mazao mengine ya nafaka na mboga mboga ilmuradi shamba linatumika kwa mwaka mzima.

Ngoja nimalize jambo hili kwa upana wake, katika sehemu ya mafunzo yetu tulienda kutembelea shamba la Jamat ambalo lina takriban ekari 80, ambapo Jamat inalima na pia kukodisha kwa wakulima wengine, Jamat ina mashamba Qadian na huko tulikoenda kutembelea. Katika mashamba haya IAAAE wamewekeza mradi mkubwa wa mfumo wa umwagiliaji wa Drip irrigation na pia wamechimba visima vinne ambavyo vinatumia umeme wa sola, hivyo mashamba haya yote hayana shida ya maji na yapo tayari kwa ajili ya kilimo kwa mwaka mzima. Kwa kuangalia unaona ardhi yao iko tambarare kabisa, akili yangu ilikuwa inaniambia labda ni asili ya ardhi ya Punjab lakini kwa kutembelea mashamba haya ya jumuiya nimejua kuwa ni kazi kubwa mno inafanyika kuandaa mashamba haya kuwa msawazo kiasi kwamba ukifungulia maji upande mmoja yanaingia na kusambaa shamba zima, tunaweza kusema ni mfumo wa majaruba wa kanda ya ziwa lakini huku ni majaruba makubwa zaidi.

Na wanafanya hivyo kwa kusambaza vilima na kuchimba vichuguu, uzuri ni kwamba wanazo mashine zote za kilimo, huku India serekali imewafanyia wakulima mfumo Fulani rafiki wa kilimo na kimiundo mbinu, na uwepo wa makampuni ya ndani yanayotengeneza matrekta na vifaa vya kilimo na mikopo ya serekali kuona trekta kila nyumba ni kiwaida. Nilikuwa naongea na jamaa ambaye anafanya kazi katika nyumba ya wageni wakati wa Jalsa, akaniuliza baba yako anafanya kazi gani nikamwambia alikuwa mkulima tu, akasema ardhi ekari ngapi nikamuambia zaidi ya ekari kumi tunazo akaruka kwa mshangao na kusema kuwa huku mtu kumiliki hata ekari mbili ni muhali ninyi mna mpaka kumi!, akasema nani kati ya ndugu zako anamsadia Mzee kulima nikamwambia baba amefariki na kila mtu anafanya mambo yake ila kaka zangu ni wakulima na wafugaji tu, nikamuuliza je wewe kwenu munamiliki ardhi akaniambia ningekuwa na ardhi ningekuwa hapa kutafuta hela ya kula, akimaanisha utajiri wa Punjab ni ardhi na kama huna basi wewe ni masikini milele, heshima na utajiri ni ardhi na kilimo kama huna ardhi wala hulimi basi ni masikini. Katika shamba la jumuiya wamepanda miwa, malimao, njegere, karoti na mboga mboga zingine lakini pia kuna kuku na mbuzi kiasi Fulani kwa kutumia mifumo ya kisasa ya mashamba darasa, ambao ni utajiri mkubwa na uwekezaji makini.

Tulifika Amritisar na kupokelewa na kuanza safari kuelekea Qadian, nilikuwa ninachokiona ni mabadiliko ya muonekana kuanzia kituo mpaka kituo, kuanzia watu waliovaa mavazi ya kawaida mpaka kuanza kuwaona waliovaa vilemba na ndevu ndefu. Alhamdulillah tulifika Qadian na mioyo, roho na matamanio kufika safari yake ya mwisho.

Baada ya kufika tulikaa katika Dar ul ziafat ambayo ni nyumba ya

Ukurasa wa 11

SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka uk. 11

wageni iliyopo karibu na Dar ul Masih, tulipewa chumba kimoja chenye vitanda vinne, tuliwakuta mashekhe wale wa Ghana wakiwa wameshapitisha siku kadhaa, tukawekwa kwenye darasa moja la masaa matatu asubuhi, ambalo ilikuwa kwa mfumo wa utambulisho wa kitabu Fulani cha Masihi aliyeahidiwa (as) au Khalifa yeyote kwa lisaa limoja, ikifuatiwa na kuangalia kuangalia video za maswali na majibu ya khalifat ul Masihi IV (rh) na khalifat ul Masihi V (aba) kwa lisaa moja na baada ya hapo ikifuatiwa na utambulisho wa idara moja ya Jamaat na jinsi inavyofanya kazi kwa saa moja pia na baada ya hapo ilifuatia ziara za maeneo matakatifu na muhimu ya Qadian na utambulisho wake kwa lisaa moja au nusu saa. Wengi walikuwa wakiniuliza upo Qadian kufanya nini niliwaambia nipo huku nasoma, walikuwa wakiniambia miaka saba haijatosha tu, bila shaka masomo haya yamekuwa na athari kubwa sana katika elimu yangu juu ya uislamu na Jamat yenyewe na athari kubwa hata kwa uimara wa imani yangu, kwani elimu ya kusoma bila kuona ina athari tofauti na ile ya kusoma na kushuhudia na kuona vitendo kwa mambo. Kwa sasa nina yakini na uzoefu wa namna fulani kwamba nikisema nasema kama mwenyeji sio msimuliwaji wa matukio.

Jambo la kushukuru kwa binafsi yangu ni kuhusu ndugu zangu niliosafiri nao, bila shaka sisi huwa hatuongei kabisa tunapokuwa nchini kwetu, kila mtu ana kazi yake, yeyote anayeona simu ya mwenzie basi anajua hio inajukumu Fulani, muda wa kuongea huwa ni wa Jalsa salana au shughuli zingine za Jamaat, ndugu zangu wananijua au tunajuana ya kwamba hata mmoja akiwa na tatizo, huwa tunaongea kujua tatizo na kumwambia cha kufanya nini kama ni kumpongeza basi anapata pongezi na kumuhakikishia kuwa tupo pamoja na kuombeana.

Ilinijia kichwani kuwa huu ndio muda sahihi wa kuondoa taarifa zisizo sahihi kichwani kuhusu baina yetu, kujuana zaidi na kujua kila mmoja ana uwezo gani rohoni mwake kiusahihi kabisa na anashauku gani, basi nilikuwa nikiingia chumbani tu, nawatupia swali nami najilaza kusikiliza namna majibu yanavyotiririka kutoka upande mmoja kwenda mwingine, ukijumuisha na uzoefu wao binafsi katika midani za kazi najikuta ni kama nimezungukwa bahari Fulani ya elimu, kadiri nilivyokuwa nikiwachimba na kuongea nao kwa pamoja au mmoja mmoja nikagundua kuwa miongoni mwetu kuna wasomi wa kina mno, lakini tunao walezi wazuri na tunao watu wanaowaza chanya, ukitugawanya utakutana na watu ambao wakisimama wawili wawili kuna wasomi na walezi wabobezi. Nasema hivyo kwa sababu walezi huwa hawana shauku ya kuongea sana bali hutenda, lakini wasomi wape mada utaona uwanja unavyotanuka na kupunguzwa sawa na haja. Kwa ukweli na kwa jina la Mungu kila mmoja kati yetu nilishakutana naye baitul dua au sehemu nyingine yeyote katika msikiti wa Mubarak au Aqsa akijishughulisha na maombi ya hali ya juu na kila mmoja alisimulia uzoefu wake na Mwenyezi Mungu.

Kirehehere changu nilitaka nijue kuwa kwanini wapo hapa. Kwa itifaki siku moja mwalimu katika kufundisha akasema kuna yeyote kati yenu ambaye dua yake imekubaliwa, hatukupata nafasi ya kujibu swali hilo kwa sababu muda uliisha, tulipofika chumbani kila mtu akafunguka kuwa ujio wake tu Qadian ni kukubaliwa kwa maombi yake, kila mtu akaeleza kisa chake cha kukubaliwa maombi, nawaza na kujisemea muandishi na labda nimeshasema kwamba nia yangu ilikuwa nikutumika kwanza ndio nifike kwenye maeneo haya, na nilipofika London na kumuona Huzoor (aba) nilifanya maombi kuwa Mwenyezi Mungu anikutanishe na watu ambao ni marafiki wangu wa kweli kwa mara ya pili na nilikuwa kuna sura muhimu nimeziwekambeleambazo nilikuwa na yakini lazima zitaenda Qadian, mmoja alikuwa Maulana Abdallah Dibah na Maulana Faiz Nasir, hawa wawili nilikuwa na yakini kwa sababu nina uswahiba nao kutoka moyoni kabisa na tukikutana kuna ulaini tunao baina yetu, na hatuwezi kuongea kwa dakika mbili bila kugubikwa na hisia. Moyoni mwangu ni kwamba Dibbah sahib atakuja Jalsa Salana kwa sababu ya MTA Africa na pia ni Sadr Khuddam USA kwa vyote hivi viwili kimoja kitamleta kwenye Jalsa, na Faiz Nasir sahib alitaka kuja Jalsa salana mwaka uliopita lakini akakosa visa hivyo niliamini mwaka huu watampa tu, kama Allah akiwakubalia hawa nami nitakuwepo Qadian. Haya njoo uone ajabu sasa, Maulana Dibbah alikuwaja Qadian lakini sio kwa ajili ya Jalsa alikuja na jopo la Khuddam pamoja na wanajumuiya wapya, naapa kwa Mungu aliponiona nikiwa mbele yake naye akitokea kwa nyuma akanitambua na kuniita kwa sauti 'Shunda how are you, you are here?…. Yaani Shunda hali yako kumbe upo hapa. Na Faiz Nasir sahib akafika wakati wa Jalsa wote tukaonana – Alhamdulillah.

Jalsa salana Qadian kwangu ilikuwa ni sehemu maalum sana katika historia ya maisha yangu kwa sababu nimekutana na marafiki zangu ambao nilisoma nao katika Jamia Ahmadiyya Int. Ghana baada ya kuachana kwa takriban miaka saba, ilikuwa ni kipindi cha muungano na kipindi cha hisia mno upande wangu kwani sikuweza kuwaangalia ndugu zangu hasa niliokuwa nao darasa moja, upendo na hisia vilikuwa vinatiririka baina yetu, Maulana Zafrullah Mustafa kutoka Cameroon aliniambia kuwa anatafuta visa kuhudhuria Jalsa salana lakini kuna usumbufu wa namna Fulani, kwani ilibidi arudi Nigeria kwa ajili ya visa kwa sababu yeye ni mzawa wa Nigeria hivyo nimkumbuke kwenye maombi, siku moja aliposti picha akiwa amevaa viatu Fulani aina ya sendo, nikamuambia ukija Qadian niletee viatu kama hivyo, ilikuwa ni sehemu ya kuuvutia moyo wangu kwa ajili ya maombi juu yake, na huo ndio mtindo wangu, kwa kuelewa ni kwamba hata kama Mwenyezi Mungu akatae maombi juu yake basi yatakubaliwa yangu kwa sababu ananiletea viatu. Yeye anamiliki duka la kutengeneza viatu kwa mikono na ushonaji wa nguo za asili. Alhamdulillah alipofika Qadian aliniletea viatu na akanipa koti lake alilotumia kwenye safari nami nililivaa katika Jalsa Salana hasa siku ya mwisho ya hotuba ya Huzoor (aba) ili kuonyesha shukurani mbele ya Mungu na kumshukuru kwa kukutanisha na ndugu yangu baada ya mda mrefu. Maulana Hafiz Azhar Nkutu wa Uganda, neema ambayo wana Afrika mashariki tunayo, jamaa ni msomi wa hali ya juu, anazungumza lugha ya kiarabu na hifizi yake ya Quran haina mfano wake, alikosa visa ya kuhudhuria Jalsa ya Uingereza lakini Allah alimfanyia wepesi kuja Qadian. Maulana Yusufu Rashid Obbat wa Kenya na Maulana Zaki Ahmad Tamuzzade ambao walikuja kwa ajili ya MTA Africa kwa ajili ya kipindi cha Messiah of the age, tukapata kupiga picha ya pamoja ya Heads of Programing MTA Afrika kutoka Afrika mashariki, hakuna cha zaidi ya kusema – Alhamdulillah

Ukarimu wa wanajumuiya wa Qadian na upendo wao kwetu ni jambo ambalo nilisipolizungumzia itakuwa ni ukosefu wa shukurani, kwa tamaduni za India hasa Punjab mtu hakuzungumzishi bila chai, kwa hivyo ni sahihi kusema hakuna kikao bila chai, Alhamdulillah chai tumezinywa sana, kwa waswahili wenzangu kuwaambia tu kwamba tumekunywa chai itakuwa ni jambo lisiloingia akilini mwao, basi hata biryani za kuku, mbuzi, na kachori na sambusa za namna mbali mbali tumelishwa. Ndugu zetu wa Kashmir wamejenga nyumba nyingi Qadian kwa sababu msimu wa mwisho wa mwaka Kashmir huwa ni msimu wa baridi kali mno na barafu huanguka, hivyo ambaye ni mwanajumuiya huja na kuishi Qadian mpaka msimu upite. Kulikuwa na mwanajumuiya mmoja ambaye alikuwa amekamilisha ujenzi wa nyumba yake, hivyo akaalika Maulamaa wa Qadian pamoja nao nasi tulialikwa kwa ajili ya dua la ufunguzi wa nyumba. Alhamdulillah nilijifunza mengi mno katika kikao kile kwani tulikaribishwa na tamtam na baada ya dua tulipewa biryani ya kuku, baada ya mazungumzo marefu walituletea chai ya chumvi ya kikashmir.

Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza Mimi kunywa chai ya namna hii, mapokeo ya namna mbali mbali yalidhihirika baina yetu, watu kukunja nyuso na miguno na mwengine kuwapa wengine chai zao, lakini hiyo haikutosha mwenyeji wetu akatuletea biskuti kwa ajili ya kunywea chai, wale waliopigwa na chai ya chumvi wakazipapatikia zile biskuti kuona labda zina sukari, lakini cha kuchekesha zilikuwa za chumvi pia, anayenijua ataniona nikiwa nacheka mno pembeni chumbani, ulikuwa ni wakati mzuri mno na uzoefu mpya. Baada ya kuondoka sehemu ile kwa furaha mno kutoka kwa wenyeji wetu ilikuwa ni nafasi nzuri ya kuwaelezea wadogo zangu waliomaliza Jamia International Ghana mwaka huu 2024, ya kwamba mwenyeji ametupa biriyani ya kuku tukafurahia mno, ilikuwa ni juu yetu kufurahia chai ya chumvi kama shukurani juu ya alichotupa mwanzo, na shukurani ni hivi kwamba usionyeshe mapokeo yoyote isipokuwa chanya mwanzo tu unapoonja kitu kutoka kwa mwenyeji wako. Mialiko mizito wakati wa karibu na baada ya Jalsa Salana ambapo tulikula na kukiangalia chakula tunachokipenda ni jambo la kujifunza mno.

Sisi wenyewe ilikuwa ni nafasi nzuri ya kujipongeza na kuonja vyakula vizuri vya India, wenzetu huku India chakula wanauza kwa kilo na kila kitu wanapima kwa mzani, hivyo tumekula kilo nyingi za kuku wa kukaanga na biryani kilo nyingi mno, tumejitoa nje kwa ajili ya kula vyakula tofauti na kuonja ladha za India.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE



TABASAMU LA KWELI LA DR. HAMIDU SHAABANI JAKA SAHIB



HABARI UK> 09

SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Na.
Sheikh Shaban Othman Shunda




Mwalimu Saleh Yassin ni mwanahistoria na muandishi wa vitabu aliyefanikiwa mno nchini kwa uandishi wake, alipohudhuria katika Jalsa salana ya Qadian nilipata kuongea naye katika hili naye akaeleza kuwa kwa kufika Qadian kulimpa uhalisia wa vitu vingi alivyovisoma kuhusu usanifu majengo wa India, kwani hata majengo ya Jamaat ni makubwa mno.

Ujenzi wa Dar ul Masih uimara wake, nakshi zake, mikunjo ya milango yake varanda na ngazi zake na jinsi unavyohama kutoka jengo moja kwenda likingine bila ya kutoka nje, Huzoor[as] aliweza kutokea dirisha moja na kurudia dirisha liningine, mfano kuingia masjid Mubarak kutoka nje kuna njia tatu mpaka nne pia pande mbali mbali acha hizo zinazotokea Darul Masih na baitul fikr na baitu dhikr. Ilinipa taswira kuwa hili ni kasri la kifalme ambalo tumepata nafasi ya kuingia na kulizuru kwa sababu tu ya kumuamini imamu wa zama, na uhalisia wake ni kweli ilikuwa ngome ya kifalme, ni wapi nitokapo, huko Dalunitanga ambapo sikuwa na kwetu bali kukulia kwa bibi na babu upande wa mama mpaka kuingia ngome ya kifalme huku nikijihisi kuwa nami ni sehemu yake bali mtumishi wa Mfalme huyu wa kiroho.

Katika majengo ya Qadian nilikuwa nahisi uimara wa mvuto wa kiroho na roho ilikuwa inatulia kwa uhalisia wake kabisa, kwani upande huu ufalme wa kiroho bado unaendelea na msaada wa Mwenyezi Mungu na radhi zake upo pamoja nao, tofauti na Jama Masjid ambapo unaona kabisa maanguko ya uislam. Ndani ya Qadian majengo yote iwe ni misikiti midogo na mikubwa, Masjid Aqsa na Minaratul Masih, nyumba za kulala wageni, majengo yote ya huduma kama kiwanda cha uchapishaji na maktaba yote yamezingatia usanifu wa hali ya juu.

Baada ya kutoka Jama Masjid tulienda sehemu fulani kwenye mgahawa unaitwa Qureshi Kabaab ili kuonja ladha ya kababu zao, wenyeji wetu walikuwa hawajafika sehemu hiyo ambayo sawa na maelezo kababu zao sina sifa mno Delhi yote, vichochoro vya Delhi ambavyo kwao ni njia rasmi ambazo unaweza ukapita na kutoboa kwenda mbali, kwa asili ya kwetu ya mitaa ya tandale na mwananyamala roho husita kwa kuona uhakika wa kupigwa ngeta nje nje ni kawaida. Lakini tulipofika kwenye ule mgahawa ooh! ilikuja yenyewe, watu wamefurika hamna nafasi, ukutani kuna picha mbali mbali za mwanzilishi na viongozi wa serekali ikionyesha kuwa huu ni mgahawa wa zamani na vijana wameendelea kurithi na kuendeleza kwani ulikuwa katika majengo mawili yaliyomkabala huko vichochoroni, lakini unapofika mgahawani shangwe lake unasahau njia uliyotumia kufika huko. Baada ya kula kababu zetu basi tulifunga safari ya kurudi Markaz pamoja na wenyeji wetu, ambapo Maulana

UK. 10



Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,000/=.

Je, Wajua?

Gravity ni hali inayofanya kitu kimoja kivute kitu au vitu vingine kukielekea. Kila kitu kina gravity, Baadhi vina gravity kubwa kuliko vingine. Vyenye gravity kubwa huvuta vyenye ndogo. Mwanadamu na kila kilichopo ardhini huvutwa kuelekea chini ya dunia kwa sababu gravity imeshinda katika vita ya mvutano. Ndio maana huwezi kurusha jiwe likaelekea juu tu bila kurudi chini. Ukiruka pia lazima utarudi chini. Vivyo hivyo, Jua lina gravity kubwa kuliko dunia, na jua huvuta dunia kuielekea. Kinachofanya dunia isivutwe na kumezwa na jua ni kwa sababu inalizunguka jua kwenye mhimili fulani. Vivyo hivyo, dunia ina gravity kubwa kuliko mwezi na ingeweza kuuvuta mwezi kama mwezi usingekuwa unaizunguka dunia. Satellite pia hazianguki duniani kwa sababu zinaizunguka dunia kwenye mhimili. Gravity inategemea ukubwa na uzito wa kitu. Mfano, uzito na ukubwa wa dunia hufanya gravity ya dunia kuwa ilivyo na jua vivyo hivyo.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com